

SIKU YA BWANA

na R. J. WIELAND

SIKU YA BWANA

NI SIKU GANI

NA

JINSI YA KUIFURAHIA

na R. J. WIELAND

Mfasiri: M. Mwamalumbili

The Lord's Day - Kiswahili

ORODHA YA YALIYOMO

Kwa

Msomaji.....
.....

Ukweli Ambao Wengi

Hawajauona.....
.

Kazi Kuu ya

Muumbaji-Mkombozi.....
.....

Ni Kitu Gani Kinachoifanya Sabato kuwa

Takatifu?.....

Sabato ni Kumbukumbu ya

Milele.....

Siku Ni Yenyewe Hasa, Njia Ndiyo

Mbaya.....
.....

Kwa Nini Evalusheni Imewanasa Watu

Wengi.....

Kwa Nini Isiwe Siku Yo

Yote.....
..

Maswali Yako

Yanajibiwa.....
.....

Kurejeshwa kwa Sabato Mahali Pake

Kulitabiriwa.....

"Wakati

Umetimia".....
.....

Jaribio la Mwisho: Alama ya

Mnyama.....

Sabato Inautia Muhuri Umoja Wako na

Kristo.....

Nyongeza: Biblia Isemavyo Juu ya Kuitunza

Sabato.....

Kwa Msomaji

Kitabu hiki kinaweza kukuondolea mzigo mzito moyoni mwako, na kukuonyesha jinsi unavyoweza kuyafurahia maisha yako kwa namna ambayo hujapata kuwazia kamwe kwamba yangewezekana kuwa hivyo. Mamilioni ya watu wanaofanya kazi ngumu katika vijiji vyetu na katika miji yetu wanaendelea kufanya kazi ngumu juma kwa juma bila kuwa na matumaini yo yote, wakijitahidi sana kujipatia maisha yao na kuchuma kiasi cha kutosha kujipatia chakula na malazi kwa ajili yao wenyewe pamoja na familia zao.

Mizigo wanayoibeba ni mizito ----- huamka mapema na kupekua [kwenda kwa miguu mitupu] kwenda kazini kwa mwendo mrefu wa kuchosha; bila hata ya kupata mshahara wa kutosha, kama inavyoonekana, ili kukidhi mahitaji yao muhimu; wakiendelea kupata hasara na kuvunjika matumaini yao; wala hawawezi kuiona nuru yo yote inayoangaza mwisho wa njia yao inayopita chini kwa chini mlimani. Kazi hiyo ya sulubu [ngumu] yenye malipo duni inaendelea siku kwa siku katika maisha yao yote.

Tunaijua ile hisia tamu tunayoipata kwa kujinyoshanyosha juu ya majani mabichi laini baada ya kumaliza kazi ya kuchosha, iletayo maumivu ya mgongo. Kila musuli na chembe hai ya mwili wa mtu hufurahia raha ya kupumzika tu.

Yesu aliyajua mambo hayo yote, maana mara nyingi alikuwa mfanya kazi aliyekakamka [aliyejitahidi sana] kubeba mbao nzito alipopanda vilima vile vya Galilaya katika kazi yake ya useremala. Yesu ndiye rafiki ya wafanya kazi wote wa ulimwengu huu walio maskini, kwa sababu ameshiriki kuibeba mizigo yao. Anajua ile hisia ya msisimko ule wa furaha unaoletwa na pumziko hilo, ambao sisi sote tunautarajia kwa shauku kubwa sana.

Walakini yeye ana hekima mno kuweza kutudanganya sisi kwa kutupatia pumziko la uongo, lile linalotoweka upesi, ambalo linatupatia tu hisia ipitayo kasi ya pumziko ili tupate kwenda tena kwenye kazi yetu ya sulubu isiyokwisha kamwe. Yeye anatupa sisi pumziko jipya tofauti: "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo,... nanyi mtapata raha nafsini mwenu" (Mathayo 11:28,29).

Raha nafsini mwetu ni raha tamu sana! Hiyo ndiyo furaha halisi ya maisha yenyewe, kitovu cha upendo, kusudi ambalo kwalo sisi tunaishi. Inayafanya maisha yetu kuwa na maana, ambayo, kwa vinginevyo, yanakuwa ya ukiwa, tena yanakuwa tupu. Inaigeuza huzuni yetu na maumivu yetu kuwa shule ya kuisimua ambamo tunajifunza siri ya furaha ile idumuyo.

"Raha" anayowapa Kristo wale wanaokuja kwake ina uwezo wa kumfanya ombaomba kuwa milionea. "Pumziko" hilo linaashiria mibaraka iliyofungamana na Sabato ya kweli ya Bwana. Na mamilioni yasiyohesabika ya watu waliochoka sana bado hawajaijua.

Iwapo mtu fulani angekupa wewe gari kubwa la mizigo lilililojaa mapesa mengi sana kiasi cha kukuwezesha kununua kila kitu unachotaka duniani humu, hiyo isingekuwa zawadi yenye thamani kama Sabato. Hiyo ndiyo siku ambayo maskini huinuliwa juu kutoka mavumbini na kuketi pamoja na wakuu, siku ambayo ombaomba anaalikwa kwenda mbali na lile lundo la takataka zake alizozikusanya ili apate kwenda kula karamu ya kitajiri mno ambayo imepata kuandaliwa kwa ajili ya mwanadamu kuweza kuifurahia. Utando wa buibui na vumbi na giza ambavyo vimeufungia mwanga wa jua usipate kuingia moyoni mwake hufagiliwa mbali kwa mng'ao unaokuja ndani ya hiyo Sabato.

Ni siku iliyotolewa kwa ajili ya kuwa na umoja na Mtu yule mwenye hekima kushinda wote katika malimwengu yote ----- yaani, Bwana Mwenyewe [Kristo]. Sabato moja tu unayoiadhimisha mbele zake inaweza kukuinua kufikia vimo vile vya juu vya maarifa yale ya kiroho na uzoefu wa maisha ambao ulikuwa hujauwazia kamwe kuwa unaweza kuwezekana kwako.

Sabato ni saruji inayozifungamanisha pamoja siku zile nyingine za juma. Inaashiria kusudi la maisha yale tunayotakiwa kuishi. Inawagawia wote uzoefu wa maisha yenye kusudi maalum, hata furaha huweza kupata nafasi ndani ya moyo wa mtu. Mibaraka inayoletwa na Sabato huinua uso, na kuyang'arisha macho yaliyokuwa yamefifia, na kuleta tabasamu moyoni. Siku zile sita za juma zipo kwa ajili ya kuifurahia Sabato! Ni maskini wasiokuwa na matumaini walioje watu wale waliokandamizwa ulimwenguni humu ambao hawaijui siku hiyo! Pengine wewe ni mmoja wa wale wanaojua kwamba wamekuwa wakiishi maisha yasiyokuwa na furaha!

Wakati ni wa thamani kuliko dhahabu au fedha. Tunaweza kuvishika vitu, na kuvisogeza hapa au pale, au hata kuviharibu. Lakini wakati ni kitu ambacho hakuna mtu awezaye kukikamata kwa mikono yake, lakini maisha yetu yanakitegemea. Sabato inatuonyesha kwamba Mungu aliumba wakati, na ya kwamba kama tutajifunza kuutumia vizuri, basi, utakuwa ni mlango wa

kuingilia katika umilele ule na kuufurahia. Mungu "ameiweka hiyo milele ndani ya mioyo yao" (Mhubiri 3:11). Hiyo inamaanisha kwamba ameweka tamaa mioyoni mwetu ya kuishi milele na kuyafurahia maisha yetu kabisa. Hiyo ndiyo sababu ya Sabato kuwa lango linalotuongoza sisi kuingia katika umilele ule wenye furaha.

Kulingana na Neno lake, hakuna mahali po pote duniani ambapo kwa wakati huu amepatenga kuwa patakatifu ----- yaani, hakuna mlima wo wote, hekalu lo lote, mti wo wote, mwamba wo wote [ulio mtakatifu]. Lakini Mungu ametenga Sabato kuwa ndio wakati mtakatifu. Kama tutakavyoona katika kitabu hiki, Sabato ndiyo ishara inayoonyesha kwamba Bwana anaingia katika maisha yetu na kututakasa, kama ule moto unaowaka kwa mwanga hafifu ndani ya kaa la moto, ukilifanya lionekane kuwa la ajabu kuliko moto huo wenyewe.

Katika nuru hiyo ya Sabato takatifu, kila mwanaume na mwanamke duniani, tajiri kwa maskini, anakuwa wa maana. Tunapovitumia vitu, tunavichakaza, tunaviharibu, tunavivunja, kisha tunavitupilia mbali. Hiyo ndiyo sababu kuna nyumba nyingi zilizovunjika na talaka nyingi siku hizi. Sabato ni mnyororo unaoifunga familia na mbingu ile yenye furaha ambako kila mtu, mweusi au mweupe, aishiye katika jumba la kifalme au aliye maskini mno kiasi cha kushindwa kununua hata viatu, mwenye hekima au mjinga, ana thamani kubwa isiyopimika mbele zake Mungu.

Hakuna mnyama ye yote kama vile mbwa au nyani au ng'ombe ajuaye cho chote juu ya kuitunza Sabato hiyo. Hawana mawazo yo yote juu ya Mungu. Lakini mamilioni ya wanadamu ulimwenguni mwetu wanaendelea kuishi kwa shida hatua moja tu juu ya maisha yote waliyo nayo wanyama. Hawainui kamwe macho yao mbinguni kuufurahia upendo wa Mungu. Yale yote wanayoyajua ni kuishi kwa anasa katika ulimwengu huu, na kwa sababu hiyo kuweza kupata maumivu yake.

Sabato ni zawadi ya thamani anayowapa Mungu wale wote wanaopenda kwa hiari yao kuingizwa katika familia yake kama wana na binti zake. Ni sawa na kurudi nyumbani kwao kila juma kwa watoto wake wanaoishi katika dunia hii ya ajabu, yaani, ya kigeni. Kwa njia ya utunzaji sahihi wa Sabato hiyo, wewe mwenyewe unajijua kuwa si mkimbizi tena mbali na nyumbani kwako halisi [mbinguni]. Unajua ya kwamba wewe "u mwenyeji" huko. Wewe si mgeni huko.

Ijapokuwa Sabato inakuja pamoja na mibaraka yote hiyo mizuri sana, Mungu hatailazimisha siku hiyo juu ya mtu ye yote. Anauheshimu uhuru wako wa kuchagua. Ingawa Mungu ndiye anayetoa, kuna jambo fulani [kwa upande wetu] tunalopaswa kulifanya: yatupasa kufanya kazi ya kupokea. Kila Sabato inayokuja kila juma huja na nafasi mpya nzuri kwetu ili tupate 'kuomba" utajiri huo kwake na tupate "kupewa". Kila Sabato inayokuja kwetu hutuacha sisi tukiwa na hekima zaidi, nguvu zaidi, na furaha zaidi. Hakuna elimu yo yote ya Chuo Kikuu ko kote kule ulimwenguni inayoweza kulinganishwa thamani yake na elimu ile anayoipokea Mtunza-Sabato [Msabato] katika maisha yake.

Fanya uchaguzi wako hivi sasa na kukoma kuwa ombaomba wakati utajiri wake Mungu unangojea upate kuupokea. Kabla hujageuza ukurasa huu, fungua moyo wako kuupokea urithi ule ambao Mungu amekuwekea. "Mimi nalikuja ili wawe na uzima," Yesu akasema, "kisha wawe nao tele" (Yohana 10:10). Ufunguo wa maisha hayo tele ni hiyo Sabato yake Bwana. Si kwamba ufunguo huo una thamani wenyewe. Thamani yake tu ni kwamba unakufungulia hazina ile unayoitaka. Kitabu hiki kitakueleza wazi kwamba Sabato yenyewe sio wokovu. Ni ufunguo tu, yaani, "ishara" au "muhuri" wa wokovu kwa njia ya imani katika Kristo. Hiyo ndiyo maana ni wa muhimu sana.

Kwa sasa unaweza kujifunza juu ya Sabato, mambo ambayo pengine hujapata kuyawazia kamwe. Kitabu hiki tayari kimekwisha kuleta maisha mapya kwa maelfu mengi ya watu kuizunguka dunia hii. Hebu sasa na wewe upate kupokea fungu lako la mibaraka hii, hilo ndilo ombi letu.

Robert J. Wieland.

SURA YA 1

Ukweli Ambao Wengi Hawajauona

=====
===

Yesu, aliyezaliwa Bethlehemu, ni Mungu Mwana tangu milele zote, Muumbaji, pamoja na Mungu Baba yake. Muumbaji wa malimwengu yote akaja hapa kama mtoto mchanga katika hori kule Bethlehemu.

Msingi wa ile kweli ni Kristo, Muumbaji, Mkombozi. Bila [msingi] huo hakuna wokovu.

Wengi hawana habari kuhusu cheo chake Kristo kuwa yeye ndiye Yule Mmoja wa Milele na Muumbaji wa vitu vyote! Mbona maarifa hayo yamekosekana? Sababu moja ni kwamba kwa kawaida watu hawayaelewi maneno ya Agano Jipya yanayomtambulisha Muumbaji huyo wa vitu vyote kuwa ndiye Kristo yule wa Bethlehemu. Waefeso 3:9, husema kwamba Mungu Baba "aliyeviumba vitu vyote kwa njia ya Yesu Kristo" [Tafsiri ya KJV]. 1 Wakorintho 8:6 husema hivi, "Mungu ni mmoja tu aliye Baba, ambaye vitu vyote vimetoka kwake, nasi tunaishi kwake; yuko na Bwana mmoja Yesu Kristo, ambaye kwake vitu vyote vimekuwapo, na sisi kwa yeye huyo." Yohana 1:10 anathibitisha kwamba Kristo ndiye Muumbaji wa ulimwengu huu: "Alikuwako ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako [kuumbwa naye]." Kristo ndiye yule Mmoja ambaye Mungu Baba alimpa kazi ile ya uumbaji wa vitu vyote.

Jambo Hilo Linazusha Maswali Maalum

Kwa nini Mungu Baba alimpa Mwanawe yule wa milele sehemu kubwa ya utendaji katika uumbaji huo? Jambo hilo linahusikaje na wokovu wetu? Je, kuna kumbukumbu inayoendelea kuuweka ukweli huo wa msingi mbele yetu?

(1) Katika fungu lile lile la kwanza la Mwanzo tunamwona Kristo kama ndiye Mungu-Muumbaji. Kisa chote cha uumbaji kinamwonyesha Kristo kuwa ndiye Bwana aliyeiumba dunia hii katika siku zile sita za mwanzo za juma lile la kwanza la wakati, na ndiye aliyepumzika siku ile ya saba.

(2) Kristo anang'aa kama taa yenye nguvu inayoangaza usiku na kuyamulika yote yanayofuata katika Agano la Kale. Kristo ndiye yule BWANA [YEHOVA] Mungu wa Ibrahimu, Isaka, na Yakobo. Yeye ndiye yule MIMI NIKO kwenye kichaka kile kilichokuwa kikiwaka moto. Ndiye Mkombozi, Kiongozi, na Mtoa-Sheria wa Israeli. Ndiye yule Bwana aliyenena kwa njia ya wale manabii (1 Petro 1:9-11).

(3) Kristo ndiye anayetawala katika Biblia yote. "Kristo ni yote, na katika yote" (Wakolosai 3:11). Kristo akasema, "Mwayachunguza [Chunguzeni] Maandiko, kwa sababu... hayo ndiyo yanayoNishuhudia" Yohana 5:39, KJV. Vitabu thelathini na tisa vya Agano la Kale hufanya kitabu kimoja cha kweli ile iliyo katika Kristo. Hivyo Yesu husema, "Katika gombo la chuo

NIMEANDIKIWA" Zaburi 40:6-8; Waebrania 10:9. Hakuna hata mmoja anayeweza kumkubali Kristo kikweli kweli katika Agano Jipya isipokuwa kama anamkubali pia katika Agano la Kale.

Kuzaliwa kwake Kristo, maisha yake yasiyo na dhambi, kifo chake kinachotupatanisha, na ufufuo wake wa ushindi, ni kweli muhimu, inayotoa ushahidi kwamba Kristo ni Mungu na Mwanadamu kweli kweli. Kristo ni Mungu Mwana tangu milele, ndiye Muumbaji wa vyote.

Yesu anatangaza, akisema: "Mimi ndimi... kweli" Yohana 14:6. Kweli yote imo ndani yake.

"Kwa ajili ya haya mimi nalikuja ulimwenguni," akasema, "ili niishuhudie kweli. Kila aliye wa hiyo kweli huisikia sauti yangu" Yohana 18:37.

Swali hili la maana sana, lisemalo, "Kweli ni nini?" hupata jibu lake ndani ya Bwana Yesu Kristo. Ndani yake Kristo "hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika" Wakolosai 2:3. Kweli yote imo ndani yake, kwa sababu yeye ndiye Kweli.

Mtu anapokuwa na ile kweli, basi, itikadi [imani] zake zote zinaunganika ndani ya Kristo. Iwapo mojawapo la maoni yake hugongana na jingine, basi, yeye hufanya uchunguzi zaidi mpaka jumla ya itikadi zake ziwe kitu kimoja [zipatane] ndani yake Kristo.

Kweli iliyo ndani yake Kristo ni kama mnyororo, na mafundisho ya injili ile ya milele ya Kristo ni viungo vyake. Mitume walizungumza juu ya habari ya ile "kweli" iokoayo na kuwatakasa wale wanaoiamini.

Ukweli ni huu, Kristo ni mali ya thamani sana awezayo kuipokea mwanadamu.

Lakini, je! hilo lina uhusiano gani na Sabato?

SURA YA 2

Kazi Kuu ya Muumbaji-Mkombozi

=====
===

Ni mtu mmoja tu aliyezaliwa humu duniani ambaye alikuwako kabla ya hapo. Huyu ndiye yule Mmoja ambaye Mungu Baba amempa

nafasi ya kwanza katika mambo yote ----- yaani, huyo Bwana Yesu Kristo. Lakini maelfu wanaomwangukia yeye kama Mwokozi wao hufikiria tu kuzaliwa kwake kule Bethlehemu na maisha yake yaliyofuata kuanzia hapo.

Tendo la Mungu la kuwaokoa wenye dhambi lilipangwa kabla ya uumbaji wa dunia hii: Mungu "ambaye alituokoa... kwa kadiri ya makusudi yake yeye na neema yake. Neema hiyo tulipewa katika Kristo Yesu tangu milele" 2 Timotheo 1:9.

Wokovu wetu ulikuwa hatarini. Ni yule tu anayeumba awezaye kuumba-upya. Kama Muumbaji, Kristo peke yake ndiye angeweza kutupatia wokovu.

Adamu alipotenda dhambi, Muumbaji wake yule akawa ndiye Mwokozi wake. Hivyo Kristo ndiye yule "Mwana-Kondoo, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya dunia" Ufunuo 13:8. (Angalia pia 1 Petro 1:18-20.)

Mwanadamu alipotenda dhambi, hakuna kiumbe [kingine] cho chote ambacho kingeweza kuyatosheleza madai ya Sheria ile ya Mungu [Amri Kumi] iliyovunjwa. Ni Mmoja tu aliye sawa na Mungu ambaye angeweza kulipa fidia kwa uvunjaji huo wa Sheria [yaani, dhambi - 1 Yohana 3:4, AJKK]. Kwa hiyo hakuna mtu ye yote, isipokuwa Bwana Yesu Kristo, Muumbaji, ambaye angeweza kujitoa nafsi yake kuwa fidia kwa ajili ya mwanadamu huyo mwenye dhambi.

Tunaweza kuokolewa tu kutoka dhambini wakati ule Kristo anapoutumia uweza wake wa uumbaji ndani ya wale waaminio: "Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya" 2 Wakorintho 5:17. Wokovu huleta uumbaji-mpya ndani ya mwenye dhambi kwa njia ya Kristo yule yule aliyemuumba mwanadamu mkamilifu hapo mwanzo. Hivyo kila mmoja anamtegemea Kristo kwa wokovu wake. Kwa kuwa yeye ndiye Muumbaji, basi, Kristo ndiye Mwokozi peke yake.

Hakuna Wokovu "Wa Kujifanyia Wewe Mwenyewe"

Wokovu ni zaidi ya msamaha wa dhambi. Kama Kristo asingefanya kitu cho chote zaidi ya kutoa msamaha wake kwetu, basi, sisi tungeweza kuendelea kutenda dhambi zile zile. Lakini neema ya Mungu ni zaidi ya msamaha wake [Kristo].

Muumini anapompokea Kristo kama Mwokozi wake kweli kweli, hapo ndipo Kristo kwa uweza wake ule wa uumbaji anamfanya [mtu huyo] kuwa mtu mpya ndani yake [Kristo] mwenyewe. Anazaliwa mara ya pili ----- safari hii anazaliwa na Mungu (Yohana 1:12,13). Kristo anampa moyo (nia) mpya.

Akiwa amemjaza na Roho wake Mtakatifu, Kristo huishi ndani ya muumini huyo maisha yake ya utii kwa zile Amri [Kumi] za Mungu [Ezekieli 11:19,20; Wagalatia 2:20). Kristo anamfanya muumini huyo kupatana na Mungu. Naye anamlinda kuwa mnyofu.

Agano la Kale linaunganisha uumbaji na wokovu ndani ya Bwana mmoja [yule yule]. "Lakini sasa, BWANA aliyekuhuluku, Ee Yakobo, yeye aliyekuumba, Ee Israeli, asema hivi, Usiogope, maana nimekukomboa; nimekuita kwa jina lako, wewe u wangu" Isaya 43:1. (Angalia pia Isaya 44:24.)

Uumbaji na Ukombozi ni kitu kimoja tu ndani ya Bwana Yesu kwa ajili ya wokovu wetu wa hakika. Kristo hawezi kugawanyika. Kumkubali Kristo kama Mwokozi ni pamoja na kumkubali yeye kama Muumbaji.

Sauli wa Tarso alipokutana na Yesu katika njia ile ya Dameski, alimtambua kama Mwokozi wake. Lakini ukweli ule unaolingiliana usemao kwamba Kristo, kwa vile yeye ndiye Muumbaji, basi, ndiye Mwokozi peke yake, ulimjia kwa ufunuo baadaye. Hapo ndipo alipokuwa chini ya uvuvio wa Roho Mtakatifu alipouandika [ukweli huo] katika nyaraka zake kwa makanisa yale machanga.

Katika waraka wake kwa Wakolosai, anasema kwamba ndani yake Kristo, "tuna ukombozi, yaani, msamaha wa dhambi" Wakolosai 1:14. Kisha anatoa sababu hii: "Kwa kuwa katika yeye vitu vyote, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi...; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake" Fungu la 16.

Sisi tunaokolewa kwa njia ya maisha makamilifu ya Kristo aliyoishi hapa duniani; kwa kifo chake kilichotupatanisha pale msalabani; kwa ufufuo wake; kwa kupaa kwake mbinguni; na kwa maombezi yake kama Kuhani wetu Mkuu kule mbinguni. Kama Yesu asingekuwa Mungu Mwana tangu milele na Muumbaji wa vyote hapo mwanzo, basi, asingeweza kuwa Mwokozi wa mwanadamu.

Kitabu cha Waebrania kinamweleza Kristo kama Muumbaji wa malimwengu yote. "Mungu... mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana,... tena kwa yeye aliufanya ulimwengu [malimwengu, KJV]" Waebrania 1:1,2.

Kumtambulisha Kristo Katika Utimilifu Wake Wote

Sura iyo hiyo inamwonyesha Baba akimwambia Mwanawe kuwa [Mwana] ndiye Mungu, Bwana [Yehova], na Muumbaji wa nchi hii: "Lakini kwa habari za Mwana [Mungu Baba] asema, Kiti chako cha enzi, Mungu, ni cha milele na milele.... Na tena, Wewe, Bwana [Yehova], hapo mwanzo uliitia misingi ya nchi, Na mbingu ni kazi za mikono yako" Waebrania 1:8-10.

Yohana pia anamtambulisha Kristo kama ndiye Mungu Mwana na Muumbaji wa ulimwengu huu: "Hapo mwanzo kulikuwako Neno [Kristo], naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu" Yohana 1:1.

Tena, "Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye

hakikufanyika cho chote kilichofanyika" Yohana 1:3.

Kutokana na picha hiyo ya nyuma Yohana anakazia uhusiano ule uliopo kati ya Uumbaji wa Kristo na Ukombozi wake.

Uweza ule ule ulioiumba dunia hii ndio ule ule unaoishikilia mahali pake. Ni kwa uweza wa Yule Neno "vitu vyote hushikana katika yeye" au hushikamana pamoja (Wakolosai 1:17). Kristo ndiye ile "Nuru halisi," ambayo humtia "nuru kila mtu, akija katika ulimwengu." "Ndani yake [Neno] ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu" Yohana 1:9,4. Ni siri jinsi mionzi ya jua inavyotoa uhai wake kwa mimea ya dunia hii. Lakini si kwa upungufu unaoonekana hakika Neno huyo, ambaye ni Kristo, anatoa uzima halisi kwako wewe na kwangu mimi.

Kumhubiri Kristo hakupaswi kuacha kumtambulisha yeye kama Mungu Mwana tangu milele na Muumbaji wa vitu vyote. Kuacha kufanya hivyo kungekuwa sawa na kujenga nyumba pasipo kuweka msingi wake.

Kwa nini wengi sana wanaomwangalia yeye kama Mwokozi wao wamesahau kipengele hiki cha Uumbaji wake Kristo? Je, njia hiyo imesahauliwa na watu wengi mno? Je, kuna ujumbe uliotoka Mbinguni kwa ajili ya siku zetu wa kuirejesha kweli hii mahali pake pa halali katika injili? Naam, upo ujumbe kama huo unaowafanya wanaume na wanawake kumjua Kristo kama Mwokozi na Rafiki yao. Unawaimarisha tena mahali pao kama wana na binti zake Mungu. Na Sabato ni sehemu ya ujumbe huo wa ajabu.

Ishara Iliyosahaulika - Sabato ya Kweli

Unaposafiri katika eneo usilolijua, unaangalia kwa makini ishara zile zilizowekwa njiani ili kuitambua barabara ile iliyonyoka kwenda kule unakotaka kwenda. Katika safari ya maisha yetu sisi pia tunahitaji kuzifuata ishara zile alizoziweka Bwana njiani mwetu. Lakini ipo ishara yake moja ambayo watu wengi sana hawaifuati. Hata hivyo, ishara hiyo iliwekwa na Kristo Muumbaji wetu hapo mwanzo.

Kama tulivyokwisha kuona, kuna kumbukumbu saba katika Agano Jipya ambazo zinamtambulisha Bwana Yesu Kristo kama Muumbaji-Mungu aliyeifanya [aliyeiumba] nchi hii kwa siku sita na kustarehe [kupumzika] siku ile ya saba. Kwa nini iwe siku ile ya saba? Si kwa sababu alikuwa amechoka sana. Neno la Mungu linatangaza kwamba "Muumba... hazimii, wala hachoki" (Isaya 40:28).

Maandiko yanatoa sababu hii:

"Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa

kwa sababu katika siku hiyo Mungu [Kristo] alistarehe akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya" Mwanzo 2:2,3.

Kristo Muumbaji alistarehe [alipumzika] siku ile ya saba ya juma lile la kwanza. Pia akaitakasa, au kuitenga kama siku takatifu. Neno la Mungu linatangaza kwamba "akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Alistarehe."

SURA YA 3

Ni Kitu Gani Kinachoifanya Sabato Kuwa Takatifu?

=====

Kustarehe [kupumzika] kwake kilikuwa ndicho kitendo cha kuitenga siku ile ya saba ya juma kama siku yake takatifu, au Siku ya Bwana kwa ajili ya mwanadamu ye yote. Siku zile sita za uumbaji ziliweka msingi wa kuitakasa [kuitenga kwa matumizi matakatifu ya ibada] siku ile ya saba kwa ajili ya mwanadamu ye yote yule.

Neno hili "Sabato," kutoka katika lugha ya Kiebrania, humaanisha pumziko. Shina la kitenzi (verb) cha Kiebrania "Shabbath" lina maana kukoma, kustarehe, ama kuitunza Sabato. Kitenzi hiki kinatokea mara mbili katika Mwanzo 2:2,3, ambako kimetafsiriwa "akastarehe." Hapo mwanzo kustarehe kwake Kristo ndiko kulikoifanya siku hiyo kuwa Siku ya Sabato.

Kristo Muumbaji anathibitisha jambo hilo katika Kutoka 20:11. Anaitambulisha siku ile ya saba kuwa ndiyo Siku ya Sabato: "BWANA akaibarikia Siku ya Sabato akaitakasa."

Bwana yule aliyezitangaza amri zile Kumi pale Sinai ni Kristo. Amri ya nne inamtambulisha yeye kama Muumbaji (Kutoka 20:8-11). Kwa hiyo kwa mujibu wa Agano Jipya, Kristo ndiye Muumbaji yule, Bwana [Yehova] aliyezitangaza amri hizo [kumi], pamoja na Baba yake.

Tena, Bwana yule aliyezitangaza zile Amri Kumi ndiye yule yule Mmoja aliyeziendeleza: "Wote [wana wa Israeli] wakanywa kinywaji kile kile cha roho; kwa maana waliunywea Mwamba wa roho uliowafuata; na Mwamba ule ulikuwa ni Kristo" 1 Wakorintho 10:1-4; angalia pia Nehemia 9:12,13.

Kristo anasema: "Ikumbuke Siku ya Sabato uitakase. Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote"

Kutoka 20:8-10.

Wengi wanadhani kwamba Jumapili ndiyo Sabato au kwamba ndiyo Siku ya Bwana. Lakini Kristo asema hivi, "Siku ya saba ni Sabato ya BWANA." Siku hiyo ya saba ni Jumamosi, sio Jumapili. Na kwa kuwa Jumapili ni siku ya kwanza ya juma, haiwezi kuwa Sabato yake Kristo, kwa sababu yeye anasema, "Siku ya saba ni Sabato ya BWANA." Kulingana na maneno hayo ya Kristo, siku ya saba (Jumamosi) ni Sabato ya BWANA [YEHOVA] Yesu Kristo, ni siku yake takatifu aliyoifanya kwa ajili ya mwanadamu awaye yote.

Wengi wamegundua tofauti iliyopo kati ya kuitunza siku ya kwanza ya juma, yaani, Jumapili, na zile Amri Kumi zinazotaka utunzaji wa siku ile ya saba. Lakini kuna njia ya kuuziba ufa huo uliotokea katika uhusiano wa mtu na Kristo: tii amri yake kwa kuitunza siku ya saba!

Mkristo amejitolea kumtii Kristo. Wokovu unaleta kwake matokeo ya utii. Hivi ndivyo ilivyoandikwa: "Akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii" Waebrania 5:9.

Bwana Yesu Kristo katika Amri zake Kumi anatuamuru kuitakasa [kuitunza] siku ya saba. Je, jambo hilo lisingemfanya kila mmoja kuitunza siku ile ya saba kwa ajili ya Bwana na Mwokozi wake?

Je! Ufufuo wa Kristo Uliifanya Jumapili kuwa Takatifu?

Wengi kwa uaminifu wanasadiki kwamba ufufuo wa Bwana wetu uliotokea siku ile ya kwanza ya juma (Jumapili) uliitakasa Jumapili kuwa siku takatifu ya kila juma. Wanadhani kwamba hiyo ndiyo sababu Jumapili imechukua mahali pa siku ile ya saba ya mwanzo (Jumamosi).

Kwa hali yo yote ile, utunzaji wa Jumapili umejengwa juu ya mapokeo ya wanadamu, sio juu ya Neno la Mungu. Hakuna po pote katika Biblia unapoweza kupata usemi unaotuambia sisi kuitunza siku ya kwanza ya juma. Maandiko huonyesha kwamba kuzikwa pamoja na ufufuo wa Bwana wetu huadhimishwa kwa njia ya ubatizo wa Kikristo (Wakolosai 2:12; Warumi 6:3-5).

Hakuna kitu cho chote ndani ya Biblia kinachoonyesha kwamba Kristo ameondoa mbaraka wake kutoka katika siku ile ya saba na kuuweka katika siku nyingine yo yote. Wanadamu hawawezi [kabisa] kufanya badiliko hilo [uhamisho huo wa siku]. Hivyo sisi tunajua ya kwamba siku ya saba, au Jumamosi, inaendelea kuwa siku ile aliyoitakasa Kristo kwa ajili ya mwanadamu.

Katika Kutoka 20:10,11 Kristo alitangaza hivi: "Siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako [sio Sabato ya Wayahudi],...

maana kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari,... akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia Siku ya Sabato akaitakasa."

Sababu hizo haziwezi kutumika kwa siku nyingine yo yote katika juma. Kwa hiyo hakuna hata moja katika siku hizo nyingine sita inayoweza kuwa badala ya hiyo [Sabato]. Kwa kuyazingazia hayo sisi tungepaswa kuitunza Sabato hiyo ya kweli ya Bwana Yesu Kristo.

Sababu hizo zinawahusu watu wote leo. Mungu hakuifanya Sabato kwa ajili ya Wayahudi peke yao, bali kwa ajili ya watu wote. Hivi ndivyo alivyosema Kristo: "Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu" Marko 2:27. Kwa kuwa ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu, basi, mwanadamu ndiye angepaswa kuitunza. Je, Mungu angeweza kufanya kitu cho chote kilicho kinyume na mwanadamu? Asingeweza kufanya hivyo kama yeye ni upendo! Sabato sio kitu kisichokuwa na msingi anachokiweka kwa nguvu juu ya mwanadamu kwa sababu tu Mungu anasema hivyo. Ni kitu cha kusitawisha maisha yake [mwanadamu] na kumfanya awe na furaha.

Kristo anaijenga amri yake hiyo juu ya tendo lake la uumbaji. Kule kuitunza siku ya saba sio amri ya Musa tu [kama watu wengi wanavyodhani] ambayo ilitolewa wakati ule wa Kutoka. Kristo Muumbaji aliitakasa, au aliitenga wakati ule wa uumbaji. Kuitunza Sabato kama vile Mungu alivyoagiza wakati ule wa uumbaji ni kukiri Uungu wake Kristo.

Sabato yake Kristo [Jumamosi] ni kumbukumbu au ishara inayoonyesha kwamba yeye ndiye Muumbaji. "Kazi itafanywa kwa siku sita; lakini siku ya saba ni Sabato ya kustarehe kabisa, takatifu kwa BWANA." "Ni ishara kati ya mimi na wana wa Israeli milele; kwani (kwa sababu) kwa siku sita BWANA alifanya mbingu na nchi, akastarehe siku ya saba na kupumzika." Kutoka 31:15,17.

Sabato Peke yake Ndiyo Siku ya Bwana

Kupitia kwa nabii Ezekieli Kristo anatangaza kwamba Sabato yake ni ishara inayoonyesha kwamba yeye ndiye Mtakasaji pia: "Tena naliwapa Sabato zangu ziwe ishara kati ya mimi na wao, wapate kujua ya kuwa mimi, BWANA, ndimi niwatakasaye" Ezekieli 20:12.

Kristo ametupa Sabato yake iwe ishara kutuonyesha kwamba yeye Ndiye anayewafanya watu kuwa watakatifu, Ndiye awaokoaye [Mwokozi] ikiwa ni nyongeza kwa kazi yake ya kuwa Muumbaji. Anaiangalia Sabato yake kama ishara inayoonyesha kwamba Yeye ndiye Mwokozi. Jambo hilo linaifunua thamani kubwa anayoiweka Kristo juu ya Sabato yake kwa ajili ya watu wake. Moyo wa sabato ni Kristo.

Haja Yetu Kubwa Sana: Kumjua Bwana

Bwana ametupa sisi siku ya saba ambayo kwayo tunatakiwa kujifunza kumjua Mwana wa Mungu kama Muumbaji-Mkombozi. Siku hiyo imeunganishwa na Kristo, kama vile uumbaji na ukombozi ulivyunganishwa naye. Kwa hiyo, kila mmoja anayempokea Bwana Yesu Kristo anapaswa kuitunza ishara hiyo ya Muumbaji-Mwokozi, yaani, Sabato yake ya siku ya saba. Kile kinachoadhimisha uumbaji kinaadhimisha pia ukombozi! [Alipumzika kaburini Siku ya Sabato baada ya kupata ushindi mkubwa dhidi ya dhambi pale Msalabani na kutupatia ukombozi kamili.]

Katika karne zile zilizofuata baada ya kipindi kile cha Mitume kumalizika, ukengeufu [upotofu] mkubwa kutoka katika ile kweli ukatokea. Utunzaji wa Jumapili, siku iliyowekwa na mwanadamu badala ya Sabato ile ya kweli ya Kristo ya siku ya saba, ukaanzishwa na kuimarishwa. Ikipokewa katika karne zote hadi katika siku hizi zetu, desturi hiyo imeleta matokeo ya watu wengi leo kuitunza Jumapili badala ya kuitunza Sabato ya Kristo ya siku ya saba [Jumamosi].

Kwa kuiweka kando Sabato yake, wanadamu wameisahau ishara ile inayomwonyesha Kristo kuwa ni Muumbaji. Mungu anatuagiza kuirejesha mahali pake ishara hiyo [Sabato] ya Muumbaji-Mkombozi katika maisha yetu ya kila siku.

Mtu anapokuja kutambua kwamba Kristo ni Muumbaji, ndipo anapoanza kuitunza siku ya saba kama ishara iliyowekwa na Mungu inayoonyesha kwamba Kristo Bwana [Yehova] anaumba na kutakasa. "Zitakaseni Sabato zangu; nazo zitakuwa ishara kati ya mimi na ninyi, mpate kujua ya kuwa mimi ndimi BWANA, Mungu wenu" Ezekeieli 20:20. Haitoshi tu kujua habari zake Bwana. Tunataka kumjua! Tunataka kujua ya kwamba yeye ni wetu, na ya kwamba sisi tumekombolewa naye, tena tu sehemu ya familia yake kweli kweli.

Mojawapo ya matatizo ya kutisha sana waliyo nayo wanadamu ni kiburi. Hebu mpumbavu ajipatie elimu kidogo, basi, yeye atatamba mbele ya wengine kana kwamba yeye ni mtu fulani mashuhuri. Hebu mlalahoi [mtu wa hali ya chini] apate kazi yenye heshima au yenye madaraka, basi, yeye ataanza kujionyesha kwa wenzake kuwa ndiye bwana mkubwa pale. Hebu mtu fukara apate fedha kiasi fulani, basi, atataka kukukoga [kujionyesha] kwazo.

Dawa inayoutibu ugonjwa huo? Kumjua Bwana: "BWANA asema hivi, Mwenye hekima asijisifu kwa sababu ya hekima yake, wala mwenye nguvu asijisifu kwa sababu ya nguvu zake, wala tajiri asijisifu kwa sababu ya utajiri wake; bali ajisifuye na ajisifu kwa sababu hii, ya kwamba ananifahamu mimi, na kunijua, ya kuwa mimi ni BWANA, nitendaye wema na hukumu, na haki" Yeremia 9:23,24.

Hapo ndipo Sabato inapoonekana kuwa ni ya maana sana ----- ni "ishara" ya ujuzi ule wa kweli, imewekwa na Bwana wetu mwenye hekima na utajiri!

SURA YA 4

Sabato Ni Kumbukumbu ya Milele

===

Wengi wanadhani kwamba utunzaji wa Sabato ya Jumamosi ulilihusu tu taifa lile la Kiebrania, na kukoma wakati ule Kristo aliposulibiwa msalabani. Wanasadiki kwamba siku ya kwanza ya juma, yaani, Jumapili, iligeuka na kuwa Siku ya Bwana kuadhimisha ukombozi kwa njia ya Kristo.

Kama Bwana Yesu angekuwa amekusudia kwamba siku ya kwanza ya juma itunzwe kwa heshima ya ufufuo wake, je! Agano Jipya lisingeweza kutupatia maelezo hayo? Lakini Agano Jipya limenyamaza kimya juu ya hoja hiyo.

Kusema kweli, kinyume chake ndicho kinachoonyesha ukweli wa mambo ulivyo. Agano Jipya linaitaja amri ya nne [Kutoka 20:8-11] kuwa inahusika na kizazi hiki kipya, kinachoishi baada ya msalaba. Kumbukumbu inatutangazia ya kwamba wafuasi wake Kristo [Wakristo waanzilishi] "walistarehe kama ilivyoamriwa (kwa mujibu wa amri ile)" Luka 23:56, KJV [Kutoka 20:8-11] siku ile iliyofuata [Jumamosi] baada ya kusulibiwa kwake [Ijumaa] wakati kizazi kile cha Musa [cha kutoa kafara za wanyama] kilipofikia mwisho wake [pale msalabani].

Pasingeweza kuwapo haja yo yote, wala sababu yo yote, wala nafasi yo yote ya kuuweka utunzaji wa siku ile ya kwanza, au Jumapili, kuadhimisha ukombozi katika Kristo. Bwana mwenyewe tayari alikuwa amekwisha kuamuru utunzaji wa siku ya saba kama ishara ya wokovu na utakaso ndani yake Kristo. Kwa hiyo, ilikuwa haipatani na mpango wake Kristo kuanzisha utunzaji wa Jumapili kama kumbukumbu ya ukombozi huo. Hiyo ilikuwa ni nyongeza isiyoidhinishwa [na Kristo].

Kristo Hawezi Kugawanyika

Watu wanapoiweka kando siku ya saba ili kuitunza Jumapili, badala ya kumheshimu Mwokozi wao wanajaribu kumtenganisha Kristo Mwokozi kutoka kwa Kristo Muumbaji. Kuiweka Jumapili mahali pa Sabato ile ya siku ya saba ni kinyume na kanuni ile ya msingi isemayo kwamba kweli yote ndani ya Kristo inafanya kitu kimoja kinachoafikiana kabisa.

Sheria zile za kafara [dhabihu za kivuli] zilizoelekeza kwa Kristo ziliondolewa pale msalabani kwa sababu Kristo alizitimiza. Kristo aka"uondoa ule uadui kwa mwili wake... ndiyo sheria ya amri zilizo katika maagizo" Waefeso 2:15. Amri Kumi zikiwa ni kanuni ya Mungu ya milele ya haki yake zinaendelea [kuwafunga watu] baada ya msalaba, kwa kadiri haki inavyoendelea kuwa haki na Mungu anavyoendelea kuwa Mungu.

Jumamosi, kama inavyohesabiwa kuanzia Ijumaa usiku wa manane mpaka Jumamosi usiku wa manane, hailingani kabisa na siku ya saba ambayo Kristo anatuagiza kuitunza. Biblia inahesabu siku ya saa ishirini na nne toka jioni hata jioni, au toka machweo hata machweo (Mwanzo 1:5,8,13,19,23,31; Marko 1:32). Sabato ile ya kivuli katika Siku ile ya Upatanisho ilishikwa

"tangu jioni hata jioni" (Mambo ya Walawi 23:32) au tangu machweo [jua lilipokuchwa au kuzama] hata machweo. Kanuni iyo hiyo inatumika katika kuanza na kuimaliza Sabato ya Bwana ya kila juma. Sabato hutunzwa kwa usahihi kuanzia jua linapokuchwa [linapozama] siku ya Ijumaa jioni mpaka jua linapokuchwa [linapozama] siku ya Jumamosi jioni.

Kristo aliwaumba Adamu na Hawa siku ile ya sita ya uumbaji wake. Ndipo siku iliyofuata akaifanya [akaiumba] Sabato kwa ajili yao. Jambo hilo linaufafanua usemi wake, usemao "Sabato ilifanyika kwa ajili ya mwanadamu" (Marko 2:27). Mungu hakukusudia kwamba iwe kwa ajili ya taifa la Wayahudi tu. Aliitenga miaka maelfu kabla hajazaliwa Myahudi wa kwanza [duniani].

Sabato Hiyo Siyo ya Musa

Kristo aliwapa Sabato hiyo wanadamu wote, kuwa kumbukumbu ya uumbaji wake. Adamu alipotenda dhambi na Muumbaji wake alipogeuka na kuwa Mwokozi wake, hapo ndipo Sabato ilipoongezewa umuhimu wake kwa kuwaelekeza watu kwa Kristo kama Mwokozi wao. Kuitunza siku ya saba hakuwezi kuwekwa katika kundi moja na sikukuu za kivuli [zilizoelekeza kwenye kifo chake Kristo] za Musa zilizotajwa katika Wakolosai 2:16,17, ambazo zilielekeza mbele kwenye msalaba na kukoma kabisa wakati ule. Sabato hii [ya siku ya saba] inapaswa kuheshimiwa milele hata milele katika nchi ile mpya inayokuja wakati ambapo dhambi haitakuwapo tena:

"Kama vile mbingu mpya na nchi mpya nitakazofanya, zitakavyokaa mbele zangu, asema BWANA, ndivyo uzao wenu na jina lenu litakavyokaa. Na itakuwa mwezi mpya hata mwezi mpya, na Sabato hata Sabato, wanadamu wote watakuja kuabudu mbele zangu, asema BWANA." Isaya 66:22,23.

Tunapolinganisha Mwanzo 2:1-3 na Kutoka 20:11 na Isaya 66:22,23, tunaiona Sabato ikifanana kama upinde wa mvua unaofanya duara lake toka uumbaji wa dunia hii hapo mwanzo mpaka dunia hii itakapoumbwa upya mwishoni. Hivyo siku ya saba ni Sabato yake Kristo kwa vizazi vyote.

Sabato inauziba ufa ule toka Paradiso ile iliyopotea hadi Paradiso ile iliyorejeshwa kwa njia ya utii wake Adamu yule wa pili, yaani, Kristo. Ni ishara ya Mungu ya "agano la milele" kati yake na watu wake milele" (Kutoka 31:16,17).

Jinsi Dhambi na Mauti Vilivyokuja

Kila Sabato inayokuja mwisho wa kila juma huonyesha pande

mbili ----- kwenda nyuma kabla ya dhambi wakati ule dunia hii ilipokuwa kamilifu; na kwenda mbele baada ya wakati ule dhambi itakapokuwa imeondolewa kabisa na dunia hii itakapokuwa kamilifu tena.

Endapo Adamu na Hawa pamoja na wazao wao wangekuwa hawajamwasi kamwe Bwana wao, basi, mambo yote humu duniani yangekuwa yameendelea kuwa makamilifu. Pasingekuwapo na uhalifu, huzuni, magonjwa, vita, dhiki, wala mauti.

Kristo Mkombozi atayafanya kuwa mapya yote yaliyopotezwa kwa njia ya dhambi. Nchi mpya itakuwa kama vile nchi [dunia] hii ambavyo ingalivyokuwa kama dhambi isingalikuwa imeingia humo. Wale wote watakaoishi katika nchi ile mpya watakuwa ni watu wenye utii wanaoishika Sabato ya siku ya saba [Wasabato watiifu] (Isaya 66:22,23). Hii inaonyesha kwamba ni muhimu kwamba watu wa Mungu waitunze Sabato sasa. Utunzaji wa Sabato hiyo ni sehemu mojawapo ya maandalizi kwa ajili ya urithi ule katika nchi ile mpya.

Kristo ameweka utunzaji wa Sabato hiyo ndani ya zile Amri Kumi. Kitendo hicho kinaifanya [amri hiyo ya Sabato] ipate kueleweka wazi kwetu kama vile ilivyo amri ile isemayo, "Usiwe na miungu mingine ila mimi" au ile isemayo, "Usiibe."

Maelfu yasiyohesabika ya watu wa Mungu walio waaminifu wameipokea injili yake Kristo, nao wanatii kwa kadiri ya nuru ile wanayoipata katika Neno la Mungu. Kwa unyofu wa moyo wanaitunza Jumapili, kwa sababu wanadhani ni sehemu ya njia ile aliyoiweka Yesu. Lakini watakapoona kutoka katika Maandiko kwamba Kristo ameiweka Sabato yake ya siku ya saba kuwa ishara inayoonyesha kwamba yeye ndiye Muumbaji na Mtakasaji, basi, upendo wao kwa Kristo utawaongoza kuikubali Sabato yake kwa furaha. Watatambua kwamba kuikubali Sabato yake ni jambo la kawaida, na lililo na sehemu muhimu katika kumpokea Kristo kama Bwana [Yehova] na Mwokozi. Injili kamili ni pamoja na kuitunza Sabato yake Kristo.

Kristo ndiye Muumbaji na Mwokozi bila kujali kama mtu ye yote anamkubali kuwa yuko hivyo. Vile vile, Sabato yake inaendelea kuwako bila kujali kama mtu ye yote anaikubali kuwa iko.

Maana ya Kiroho ya Sabato

Sabato haiwezi kuwa ishara ya Yesu Mtakasaji katika maisha ya mtu awaye yote isipokuwa kama Kristo anamtakasa kwa kuwako kwake ndani ya mtu huyo. Hakuna ye yote awezaye kuitunza Sabato mpaka awe amezaliwa mara ya pili, na kuwa na Yesu aishiye ndani ya moyo wake. Utunzaji wa Sabato ni zaidi ya kuacha kufanya kazi ya kawaida siku ile ya Jumamosi. Ni wale tu ambao wanatakaswa kila siku ndani ya Kristo wawezao kuitakasa siku hiyo takatifu ya Kristo.

Kristo anasema hivi: "Tena naliwapa Sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao, wapate kujua ya kuwa mimi, BWANA, ndimi niwatakasaye" Ezekeieli 20:12.

Ku"takaswa" maana yake kupewa roho mpya. Hatuendelei tena kuchagua kukasirika, wala kupaza sauti zetu na kutamka maneno yaliyo mabaya, yanayochukiza, yaani, yaliyo machafu. Tunachagua kuwa waaminifu hata kama hakuna mtu ye yote anayetuangalia. Tunachagua, katika Kristo, kuitunza miili yetu kama Hekalu la Roho Mtakatifu. Tunaupa kisogo uchoyo wetu, mambo yetu machafu kama vile uasherati na uzinzi. Damu yake Kristo inausafisha moyo wetu wenye dhambi, ili upate kuwa safi. Anaiondolea mbali hatia ile ya zamani ambayo imezisumisha roho zetu. Bwana anasema kwamba Sabato yake ni "ishara" ya kazi yake hiyo [ya utakaso] inayoleta furaha.

Kuigundua Raha ya Sabato

Umbaji na Ukombozi huonyesha upendo wa Mungu wa milele kwa wanadamu. Na Sabato hiyo ni ishara pia ya upendo huo wa Mungu. Muumini anapoelewa kweli hiyo, hapo ndipo upendo wa Kristo unapomwongoza kuitunza Sabato hiyo ya siku ya saba kwa heshima inayoonyesha upendo wake kwa Kristo kama Muumbaji-Mkombozi wake. Sabato inakuwa kiungo kimojawapo cha upendo, kinachomwunganisha muumini huyo na Bwana wake.

Upendo wa Mungu ndani yake yule muumini unaonekana katika utii wake kwa amri zake [kumi]: "Mtu asiyenipenda, yeye hayashiki maneno yangu" Yohana 14:15,21,24.

Yule anayeuruhusu moyo wake ili upate kujazwa na upendo wa Mungu hahitaji kusukumwa ili apate kutii. Tamaa yake inayomwongoza ni hii: "Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, Sheria yako [Amri Kumi] imo moyoni mwangu" Zaburi 40:8.

Hakuna mwanaume au mwanamke ye yote awezaye kuupokea upendo wake Kristo bila kuurudisha kwake. "Sisi twapenda kwa maana yeye alitupenda sisi kwanza" (1 Yohana 4:19). Ndani ya muumini upendo huo kwa hakika utazaa utii kwa amri [kumi] za Mungu.

Bwana anaunganisha kujifurahisha katika Bwana na utunzaji wa Sabato yake na kuiita kuwa ni siku ya "furaha" Isaya 58:13,14. Pia, anaunganisha utunzaji wa Sabato yake na kuyachagua mambo yale yanayompendeza (Isaya 56:2-5). Kwa kuwa Sabato ni siku ya mbingu kuwa hapa chini, basi, hiyo inakuwa ni siku ya furaha kuliko zote katika juma.

Na Tuzifuate Nyayo Zake Yesu

Yesu alisema, Mimi Ndimi njia" Yohana 14:6. Yeye peke yake ndiye njia halisi ya kwenda mbinguni. Kristo alipoishi hapa duniani aliitunza siku ya saba kwa uaminifu, siku ambayo yeye kama Muumbaji aliitenga kwa ajili ya mwanadamu mwisho wa kazi yake ya uumbaji. Hivyo Kristo akatuachia sisi "kielelezo [tu]fuate nyayo zake" 1 Petro 2:21. Mojawapo ya "nyayo" [hatua] hizo ni kuitunza siku ya saba kama vile alivyofanya yeye. Furaha yake inakuwa furaha yetu.

Warumi walioitawala Palestina walikuwa na majina yao kwa siku kadhaa za juma. Siku ya saba ya juma waliipa jina la Sarateni, siku ambayo sasa tunajua kwa jina la Jumamosi (Saturday). Utunzaji wa siku ya Jumapili uliongezwa na wanadamu baada ya kufa wale mitume. Lakini Mungu anatutaka sisi kugeuka na kuyaacha mambo yote yaliyoongezwa na wanadamu [ambayo hayamo katika Biblia].

Ufunuo 14:6-14 huonyesha kwamba Mungu atakuwa na watu wake waliosalia wanaotambulikana kama "hao wazishikao amri [kumi] za Mungu na imani ya Yesu" Ufunuo 14:12. Amri zake zote [kumi] ni kwa faida yako sikuzote (Kumbukumbu la Torati 6:25). Sabato haitakuchukulia wakati wako kwa shughuli zako zile nyingine, bali itakupa wakati wa kudumisha ushirika wako na Mungu, kuyainua macho yako kutoka katika mambo yako ya muda ya maisha haya na kuyakaza juu ya mambo yale ya milele yenye thamani.

Hakuna mtu ye yote asiyekuwa muumini, bila kujali maazimio yake aliyoyaweka, awezaye kujizua kusema maneno yake mwenyewe katika siku ile ya Sabato. Kusema kweli hana ari yo yote ya kufanya hivyo. Ni mtu yule tu aliyeongoka kweli kweli awezaye kuitunza Sabato. Utunzaji wa Sabato wa kweli kwa njia hiyo ni ishara ya uzoefu wa kweli wa maisha ya Kikristo.

Nia yake huunganishwa na nia ya Kristo, mapenzi yake [muumini huyo] huunganishwa na mapenzi yake [Kristo]. Hapo ndipo Sabato haitakuwa mzigo wala ya kuchosha kwake, bali itadhihirisha furaha ya kweli ile idumuyo, yaani, ishara ya ahadi yake ya kumtakasa kila mtu anayempokea yeye.

SURA YA 5

Siku Ni Yenyewe Hasa, Njia Ndiyo Mbaya

=====
===

Wayahudi waliitunza siku yenyewe hasa, ila waliitunza kwa njia mbaya. Walimshtaki Kristo kwamba alivunja Sabato, kwa sababu yeye aliwaponya wagonjwa siku hiyo, na kutangaza kwamba ilikuwa ni halali kutenda mema siku ya Sabato (Mathayo 12:12).

Walikuwa wameifukia Sabato chini ya maagizo makali yanayovuka mpaka ambayo walikuwa wameyatunga [wenyewe]. Wakaifanya Sabato kuwa siku ya kuwakosesha watu raha na isiyopendeza kwao. Lakini Kristo aliiweka Sabato kuwa siku ya furaha, iliyojaa roho tamu ya furaha ile takatifu.

Waliitunza Sabato ili kujipatia haki yao wenyewe, jambo ambalo haliwezekani kabisa. Haki inayokubalika inapatikana tu kwa njia ile ya kuipokea haki ya Kristo kwa imani.

Utunzaji sahihi wa Sabato shina lake ni katika haki yake Kristo inayopokewa kwa imani. Lakini dhana ya Wayahudi ya utunzaji wa Sabato ilitokana na mfumo ule potofu wa haki kwa njia ya matendo. Wakiwa wameifanya Sabato kuwa siku yao ya mapumziko hawakuweza kuingia katika raha ya Bwana.

Utunzaji sahihi wa Sabato unalikusisha pumziko la kiroho ndani yake Kristo, linalowezezana tu wakati ule mtu anapopata uzoefu ule wa haki kwa njia ya imani. Usemi huu "Siku ya saba ni Sabato ya BWANA" una maana iliyo sawa na "siku ya saba ni raha ya BWANA."

Sura ya nne ya Waebrania inahusu usemi wa Mungu juu ya siku hiyo ya saba: "Mungu alistarehe siku ya saba" Waebrania 4:4. Mtu yule aliyeongoka [aliyebadilika na kuwa na tabia nyofu] ambaye ameingia katika raha yake Mungu amestarehe pia katika kazi zake, kama vile Mungu alivyostarehe katika kazi zake (Waebrania 4:10).

Pumziko Lenye Mibaraka ni Kristo Peke Yake Awezaye Kutoa

Yesu anaturalika, akisema, "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha"

(Mathayo 11:28). Neno la Kiyunani lenye maana ya "nitawapumzisha" ni lile lile lililotumika kuhusiana na utunzaji wa Sabato katika Waebrania 4:4,9-11. Kwa maneno mengine, Yesu anawaahidi watu wale waliochoka sana, wanaofanya kazi za sulubu [ngumu], wasiotosheka [na maisha haya kama yalivyo] kwamba atawapa raha kamili ya pumziko lao la kiroho linalokuja kwa njia ya kuitunza Sabato. "Nanyi mtapata raha nafsini mwenu," asema yeye, sio pumziko tu la kimwili kama lile la mnyama anayelala usingizi. Ni pumziko lile linalotokana na kuondolewa mizigo yetu mizito inayoilemea mioyo yetu.

Hakuna hata mmoja awezaye kuingia katika raha yake Kristo mpaka awe ameacha kabisa kujaribu kujiokoa mwenyewe kwa matendo yake. Badala yake, amruhusu Kristo kufanya kazi ndani yake kile kinachopendeza machoni pake. Utunzaji sahihi wa Sabato unaashiria kwamba Kristo amemfanya Mtunza-Sabato huyo kuwa mtu mpya, na kule kuwako kwake ndani yake [mtu huyo] humtakasa kila siku. Utunzaji pekee wa Sabato unaokidhi matakwa ya Mungu ni wa aina ile ambayo utunzaji wa siku ya saba ni ishara ya uzoefu wa haki katika maisha ya muumini huyo ndani yake Kristo.

Kweli zile zilizo nusu-nusu ni za hatari sana kuliko mafundisho yale ambayo yamejaa karibu makosa matupu. Maandiko fulani yanapochanganywa na makosa, basi, hutumika kuleta picha ya kuhalalisha makosa hayo kwa wale wasioyajua mafundisho ya kweli ya Biblia. Yatupasa kuhakikisha kwamba tunayo kweli yote ndani ya Kristo.

Wengine husema hivi, "Kwa kuwa wokovu ni kwa neema tu, basi, sisi hatupaswi kuitunza siku ya saba." Sehemu ya kwanza ya usemi huo ni sahihi. Lakini sehemu yake ya pili haipatani na Maandiko na kwa hiyo ni kosa.

Chini ya Sheria Kinyume na Chini ya Neema

Mtu yule aliyeongoka hayuko chini ya lawama ya sheria, bali chini ya neema. Maisha yake hayatawaliwi tena na dhambi, au uvunjaji wa sheria [Amri Kumi]. "Kwa maana dhambi [uvunjaji wa sheria] haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya [lawama ya] sheria, bali chini ya neema [msamaha]. Ni nini basi? Tufanye dhambi [tuvunje sheria] kwa sababu hatuwi chini ya [lawama ya] sheria bali chini ya neema [msamaha]? Hasha!" Warumi 6:14,15.

Kule kuwa chini ya neema [msamaha] hakumpi mtu ye yote haki ya kuiba, kusema uongo, au kuvunja sehemu yo yote ya sheria ile [Amri Kumi] ambayo Sabato ya siku ya saba ni sehemu yake. Kinyume chake neema ya Mungu hutia moyo mpya, au mawazo mapya, ndani ya mwenye dhambi [mvunja sheria] yule aliyetubu, ili apate kuzitii amri [kumi] za Mungu (Ezekieli 11:19,20).

Je! wale wanaoishika siku ile ya saba ni watu wanaotaka kuokolewa kwa sheria? Je! wameanguka katika hali ya neema?

Kushika Sheria [Amri Kumi] kwa lengo la kuokolewa kwayo ni kuitii Sheria hiyo na mambo fulani yanayopasa kama njia ya kuhesabiwa haki mbele za Mungu. Ushikaji wa Sheria [Amri Kumi] kama huo ni makosa, kwa vile kuhesabiwa haki huja tu kwa njia ya imani katika Kristo.

Utii kwa kila amri ya Bwana ni matokeo ya haki ya Kristo iliyopokewa kwa njia ya imani. Chini ya Agano Jipya la Neema Mungu huziandika amri zile [kumi] moyoni (Waebrania 8:8-10; [Kutoka 20:3-17]).

Utunzaji huo wa Sabato haumfanyi mtu kuwa mshika sheria kwa lengo la kujipatia wokovu kama vile kulivyo kule kuzishika amri zile tisa [zilizobaki]. John Wesley alikuwa sawa aliposema kwamba baada ya kuongoka kwake Sheria [Amri Kumi] ipate kumtunza yeye ili adumu kukaa ndani ya Kristo kama vile alivyoitaka [Sheria hiyo] kumleta kwa Kristo.

Utunzaji huo wa siku ya saba haupingani na wokovu kwa neema hiyo inayotolewa bure. Kinyume chake, ni ishara kwamba waumini hao wameokolewa kwa neema hiyo inayotolewa bure. Utunzaji sahihi wa Sabato ni ishara kwamba neema ya Mungu inafanya kazi ya kumtakasa muumini huyo aliyehesabiwa haki ndani ya Kristo. Unaashiria kwamba mtu huyo hawezi kujiokoa wala kujitakasa mwenyewe kwa matendo yake.

Dini ile ya Kiyahudi wakati ule wa Kristo ilifuata ushikaji wa nje tu wa andiko lile la sheria ili kujipatia sifa ya kupata wokovu, wakiwa na maono kidogo mno juu ya hali ile yenye kina sana, yaani, ya ndani sana ya kiroho ya Sheria ile [Amri Kumi]. Kwa kulinganisha na hali hiyo, imani ya kweli huenda mbali zaidi ya andiko la sheria kwa kuzaa utii ule wa ndani sana wa kiroho wa Sheria hiyo. Utii kama huo sio njia ya kujipatia wokovu, bali ni tunda la [matokeo ya] neema katika maisha ya mtu huyo. Tunaishi "katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya andiko" Warumi 7:6.

Hotuba ya Kristo Juu ya Mlima

Wayahudi walifikiri kwamba utii kwa amri ile isemayo "Usiue" ulikuwa ni ule wa kujizuia tu kutenda kitendo halisi cha kuua. Lakini Yesu akawaonyesha kwamba kule kuwa na chuki dhidi ya mtu ye yote kulikuwa ndiko kuivunja amri hiyo. Hali yake ya kiroho ni hii: Mpende jirani yako, hata adui yako, kama nafsi yako.

Je! kuishi "katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya andiko" maana yake ni kwamba mtu anaweza kulivunja andiko la Sheria hiyo [Amri Kumi] wakati angali bado anaitii hali yake ya kiroho? Wengine hudai kwamba "si katika hali ya zamani, ya andiko" ati humaanisha siku ile halisi, yaani, ya saba, kama ilivyotajwa katika amri hiyo [Kutoka 20:8-11] kwamba haina haja ya kutunzwa, na ya kwamba "katika hali mpya ya roho"

ati humanisha kwamba utunzaji wa Jumapili ndio unaotekeleza hali ya kiroho ya amri hiyo.

Mtu anaweza kulifuata andiko la Sheria, wala asiweze kutii hali ya kiroho ya Sheria hiyo. Lakini hakuna mtu ye yote anayeitii hali ya kiroho ya Sheria hiyo awezaye kuishi kinyume cha andiko hilo [la Sheria]. Hebu fikiria juu ya amri ile ya sita, isemayo, "Usiue." Iwapo mtu mmoja anawapenda maadui zake, na jirani yake kama nafsi yake, basi, kulingana na hali ya kiroho ya amri ile ya sita, kamwe hataweza kwenda kinyume na andiko lake na kumwua mtu.

Kuishi "katika hali mpya ya roho, si katika hali ya zamani, ya andiko" kunahusu utunzaji sahihi wa Sabato, kama vile alivyofanya Yesu, wala si katika hali ya zamani, ya andiko kama walivyofanya Wayahudi ambao waliishika Sheria [Amri Kumi] kama njia ya kupatia wokovu wao.

SURA YA 6

Kwa Nini Evalusheni Imewanasa Watu Wengi

=====
===

Laiti kama Sabato ingalikuwa imetunzwa kwa uaminifu, ingekuwa kizuizi kinachofaa kabisa dhidi ya mafundisho potofu na ibada ya uongo.

Hapawezi kuwapo na nyumba bila mjenzi. Biblia inataja kuwako kwa dunia hii kama ndio ushahidi kwamba yuko Muumbaji-Mungu (Warumi 1:20).

Muumbaji-Mungu huyo ndiye Mungu wa Kweli peke yake, kwa kuwa ile yote inayoitwa miungu haina uwezo kabisa wa kuumba (Zaburi 96:5; Yeremia 10:10-12). Muumbaji huyo kwa hiyo anapaswa kuabudiwa kabisa, yeye peke yake.

Mungu Baba alimpa Mwanawe Kristo kazi ile ya uumbaji wa vitu vyote. Yeye [Kristo] aliifanya [aliiumba] dunia hii kwa siku sita, na kupumzika siku ile ya saba. Kwa vile Sabato inaelekeza kwa Muumbaji huyo kuwa ndiye Mungu wa Kweli, basi, utunzaji wa siku ya saba umeunganishwa na ibada ya kweli ya Baba na Mwana [Yohana 4:22-26].

Ipo tofauti dhahiri kati ya Muumbaji na viumbe vyake. Sabato inaiweka tofauti hiyo mbele yetu daima. Hivyo utunzaji wa Sabato kama vile Bwana anavyoamuru, ni alama ya kuwabainisha waabudu wa kweli wa Mungu yule wa Pekee wa Kweli.

Fundisho potofu lililoenea mbali sana linashikilia kwamba kila moja ya siku zile sita za uumbaji katika kitabu cha Mwanzo Sura ile ya Kwanza haikuwa siku ya saa ishirini na nne bali kwamba kilikuwa ni kipindi kirefu cha wakati, labda mamilioni ya miaka.

Biblia inaonyesha kwamba hizo zilikuwa ni siku halisi za saa ishirini na nne kila moja, ambazo zilihesabiwa kutoka jioni moja hata jioni iliyofuata (Mwanzo 1:5,8,13,19,23,31). Siku ya saa ishirini na nne inakadiriwa kutokana na muda inaotumia dunia hii kuuzunguka mara moja mhimili wake, (hiyo ndiyo "jioni ikawa asubuhi" ya Mwanzo Sura ya Kwanza). Mwaka wa siku mia tatu sitini na tano unakadiriwa kwa muda uliotumika kwa dunia hii kulizunguka jua katika mzunguko wake mmoja. Mwezi unakadiriwa kwa takriban muda unaotumia mwezi kuizunguka mara moja dunia hii.

Juma la Siku Saba Linatoka Wapi?

Hakuna kitu cho chote katika maumbile kinachoweza kutoa sababu ya kuwako kwalo. Chimbuko lake linatokana na uumbaji wa dunia hii kwa siku sita, na lile pumziko la Muumbaji wetu siku ile ya saba. Miaka maelfu baada ya uumbaji juma hilo la siku saba bado huonyesha kwamba juma la uumbaji lilikuwa na urefu wa masaa [saa] 168, kama kila juma tangu wakati ule lilivyo nayo.

Kutoka 20:8-11 inalithibitisha jambo hilo. Bwana anatutaka sisi kufanya kazi siku sita na kupumzika siku ya saba, maana kwa siku sita alifanya nchi [dunia] na kustarehe siku ile ya saba. Amri hiyo inaonyesha kwamba siku zile sita za uumbaji zilikuwa ni siku zile zile anazotupa kwa ajili ya kufanya mambo yetu kila juma.

Hakuna hata mmoja awezaye kuitunza siku hiyo ya saba kama Kristo anavyoamuru na wakati uo huo akawa akiamini ya kwamba ilichukua miaka mamilioni kwa mwanadamu kujitokeza kutoka katika viumbe vile vya hali ya chini vyenye uhai. Utunzaji wa Sabato

yake Kristo unamfunga mtu huyo kuamini uumbaji wa dunia hii katika siku halisi sita, yaani, siku za saa ishirini na nne kila moja. Nadharia hiyo ya Evalusheni [isemayo kwamba mwanadamu alitokea katika vyumbe duni au viumbe vimetokea vyenyewe tu] ni jaribio mojawapo la Shetani la kuharibu msingi ule uliokwisha kuwekwa na Mungu wa kuitunza Sabato hiyo ya kweli, yaani, mpango wake wa kuwakengeusha watu kutoka katika kweli kama ilivyo ndani ya Kristo.

Siku hiyo iliyowekwa na mwanadamu, yaani, Jumapili, iliunyang'anya ulimwengu mzima kinga ya Bwana dhidi ya fundisho hilo potofu la Evalusheni [Evolution]. Kuikubali siku hiyo ya badala kulikoenea mbali kulifanya iwe rahisi kwa wengi kudanganyika.

"Imani pasipo matendo haizai [imekufa]" Yakobo 2:20. Amri ya Kristo ya Sabato inathibitisha kwamba utunzaji wa siku ya saba ni njia iliyochaguliwa na mbingu ya kuonyesha imani yetu katika uumbaji wa dunia hii kwa siku halisi sita, yaani, siku za saa ishirini na nne kila moja.

Wale wote wanaoamini katika uumbaji uliochukua siku sita zenye masaa ishirini na nne kila moja wanapaswa kuionyesha imani yao hiyo kwa kuitunza Sabato ya siku ya saba ya Kristo. Miongoni mwa halaiki ya wale wanaoitunza siku ya Jumapili, wengi hawaikubali nadharia hiyo ya evalusheni. Wanadumisha imani yao katika uumbaji wa dunia hii kwa siku sita zenye saa ishirini na nne kila moja. Kadiri nuru inavyozidi kung'aa kutoka katika Neno la Mungu, wengi wao wataona kwamba utunzaji wa siku ya saba ni njia aliyoiweka Kristo ili wapate kuonyesha imani yao katika uumbaji wake wa dunia hii katika siku sita.

Watu Waliookolewa Kwa Neema Waukubali Uumbaji na Sabato

Utunzaji wa Sabato ya siku ya saba ya Kristo huwatenga kwa nguvu wale wanaokubali uumbaji kwa siku zile sita za Mwanzo Sura ya Kwanza na wale wanaoitunza Jumapili na kuikubali [nadharia ya] evalusheni. Sabato na siku zile sita za uumbaji katika mwanzo Sura ya kwanza haviwezi kutenganishwa kabisa.

Kwa upande mwingine, kuiweka kando Sabato na kupendelea kuitunza Jumapili ni kuziweka kando siku zile sita za uumbaji katika Mwanzo Sura ya Kwanza. Kwa hiyo, hiari [uchaguzi] kati ya mambo hayo mawili iliyojengwa juu ya Maandiko kwa kila mmoja anayeitunza Jumapili na bado anaamini juu ya uumbaji [wa Mungu] ni kuitunza siku ya saba kama Kristo anavyoamuru.

Endapo Sabato itapoteza mvuto wake uliokusudiwa, basi, amri zote zilizobaki katika zile Kumi ni batili pia, kwa sababu amri ya Kristo inayohusu Sabato inaitia "muhuri" sheria hiyo [Amri Kumi - Isaya 8:16]. Inawakilisha mamlaka yake Mungu.

Kwa Nini Shetani Anaichukia Sabato

Kama Kristo Muumbaji anafutiliwa mbali kwa kuikataa Sura ile ya Kwanza ya kitabu cha Mwanzo, basi, msingi huo unaondolewa kwa Kristo na kumwacha kama Mwokozi peke yake. Iwapo Muumbaji si Mkombozi pia, basi, mpango ule wa wokovu ungeweza kushindwa kabisa. Ni nani kama si Muumbaji huyo awezaye kumuumba upya mwanadamu na kumrudisha katika hali yake ile ya kwanza? Kupitia kwa nabii Ezeieli Kristo anasema, "Zitakaseni Sabato zangu; nazo zitakuwa ishara kati ya mimi na ninyi,... mimi ndimi BWANA [YEHOVA], Mungu wenu" Ezeieli 20:20.

Makumi ya maelfu humsifu Kristo kuwa ni mtu mwema sana na Mwalimu Mkuu kushinda wote. Lakini hawamheshimu yeye kama ndiye Mungu wa Kweli. Ukengeufu huo kutoka katika kweli usingeweza kutokea kamwe kama wangukuwa wameendelea kuitunza Sabato ya kweli ya Kristo. Kila mmoja anayeitunza siku ya saba kama anavyoamuru Kristo anakiri kabisa kwa kitendo hicho Uungu wake Kristo kama ndiye Mungu Mwana, Muumbaji wa vitu vyote.

Hakuna Haja Ya Kuiamini Evalusheni!

Kwa nasibu, yatupasa kuzingatia ukweli kwamba Evalusheni sio ukweli uliokwisha kuthibitishwa. Ni nadharia [dhana] tu, ambayo imejengwa juu ya kumbukumbu za kijiolojia [elimu ya kuchunguza mawe, udongo na uso wa dunia] ambazo zinaweza kuelezwa kwa utoshelevu zaidi kwa kutumia kumbukumbu ile ya uumbaji iliyo katika Biblia pamoja na Gharika ile ya Nuhu.

Mwanamatengenezo ya Kanisa, John Calvin, alisema hivi: "Chini ya pumziko la siku hiyo ya saba, Mtoa-Sheria huyo wa Kimbingu alimaanisha kuwapa wana wa Israeli mfano wa pumziko la kiroho ambalo kwalo waumini walipaswa kuachana na kazi zao [matendo yao mabaya] na kumruhusu Mungu kufanya kazi ndani yao.... Yatupasa kupumzika kabisa ili Mungu apate kufanya kazi ndani yetu" (Institutes, Vol. 11, uk. 339,340).

Naam, kwa njia ya sabato hiyo, sisi tunajisalimisha nafsi zetu kabisa kwa Bwana na kujiweka mikononi mwake, kama watumishi wake.

Sabato ni siku ya Mungu inayowaweka wanadamu wote katika usawa. Mgawanyo wa jamii usiokuwa na usawa unasawazishwa kila juma Sabato inapokuja. Maskini, matajiri, wasomi na wajinga, wakuu kwa wadogo, wote hukusanyika kama familia moja kumwabudu Bwana katika siku yake hiyo takatifu.

SURA YA 7

Kwa Nini Isiwe Siku Yo Yote?

=====
===

Je, inaleta tofauti yo yote ile, kama ipo, kuhusu siku gani anayoitunza mtu? Bwana amemwacha kila mtu huru kuchagua iwapo atamtii yeye au hatamtii.

Lakini hilo halina maana kwamba siku yo yote wanadamu wanayoweza kuchagua kuitunza ni siku sahihi kulingana na Sheria ya Mungu [Amri Kumi]. Katika Kutoka 20:8-11, Kristo Muumbaji amekata maneno kwa kusema kwamba siku ya saba tu ndiyo siku sahihi kwa mujibu wa Sheria yake [Amri Kumi]. Kuweka siku nyingine yo yote badala yake ni uasi [uvunjaji wa Amri zote Kumi - Yakobo 2:10-12]. Utunzaji wa Sabato hiyo [ya Kristo] hauwezi kugeuzwa na kuwa utunzaji wa siku moja yo yote katika zile saba.

Miaka elfu sita ya mateso imewaathiri vibaya sana wanadamu [Isaya 24:1-6,19,20] kwa sababu Adamu na Hawa walilikubali shauri la yule mwovu kwamba isingeleta tofauti yo yote iwapo wangekula matunda ya mti ule ambao Bwana alihifadhi au ya mti mwingine wo wote bustanini mle.

Siku ipi tutakayoitunza ----- Jumapili, Jumamosi, au siku nyingine yo yote ----- si suala linalohusu tu uchaguzi wa siku gani tutakayoitunza. Hoja ya msingi ni utii kwake Kristo dhidi ya uasi kwake. Je, tutaendelea kuwa na mungu mwingine mbele zake Bwana? Je, tutamtii Bwana na kushika siku yake ile aliyoiamuru? Au tutatii desturi na mapokeo ya wanadamu?

Je! Paulo Anaruhusu Utunzaji wa Siku Nyingine Yo yote Anayoichagua Mtu?

"Mtu mmoja afanya tofauti kati ya siku na siku; mwingine aona siku zote kuwa sawasawa. Kila mtu na athibitike katika akili zake mwenyewe. Yeye aadhimishaye siku, huiadhimisha kwa Bwana; [naye asiyeiadhimisha siku, kwa Bwana haiadhimishi]" Warumi 14:5,6 [Tafsiri ya KJV].

Kristo aliuhifadhi sana utunzaji wa siku ya saba miongoni mwa Amri zile Kumi takatifu zidumuzo milele zote. Jambo hilo linathibitisha kwamba hapawezi kuwapo na kitu kingine cho chote katika Maandiko kilicho kinyume na utunzaji wa siku hiyo ya saba kama Sabato yake Kristo.

Paulo alimfuata Yesu katika utunzaji wa siku hiyo ya saba kwa kuitakasa [Matendo 17:1-4; 18:1-4; 16:13,16]. Paulo pia alimfuata Yesu katika kufundisha kwamba Amri zote Kumi zinapaswa kutiiwa (Waefeso 6:2; Warumi 7:7,12; 3:31; 13:8,9). Iwapo katika Warumi 14:5,6, Paulo alikuwa anaruhusu utunzaji wa siku nyingine yo yote, basi, angekuwa anaipinga mojawapo ya Amri Kumi za Kristo. Pia angekuwa ameyakanusha mafundisho yake mwenyewe. Walakini ukinzani [ubishi] huo haupo hapo wala sio hoja iliyopo katika Warumi 14:5,6 [sio kuchagua siku yo yote ya kuabudu].

Yatupasa kuzingatia hali iliyokuwako kule Rumi miongoni mwa waumini wa Kiyahudi na wale wa Mataifa. Chini ya Sheria ya Kafara [dhabihu] Wayahudi walitakiwa kuzitunza sabato saba [za kivuli] za kila mwaka (kama siku za mapumziko) ambazo zilihusiana na Pasaka [siku ya 15 na ya 21 ya mwezi wa kwanza - Law.23:7,8), Pentekoste [siku ya 50 - Law.23:16,21], Sikukuu ya Vibanda [siku ya 15 na ya 22 ya mwezi wa saba - Law.23:34-36], na Siku ya Upatanisho [siku ya 1 na ya 10 ya mwezi wa saba - Law.23:24-32]. Hizo [Sabato za tarehe au siku maalum] zilikuwa tofauti na Sabato ile ya juma [Law.23:3] ambayo imo katika zile Amri Kumi. Angalia Mambo ya Walawi 23:3-38 [linganisha na Law.23:3; Kutoka 20:8-11].

Pamoja na maadhimisho mengine [ya dhabihu], sikukuu hizo na sabato zake [saba] za mwaka [za kivuli] ziliondolewa na kugongomewa msalabani (Wakolosai 2:14-17). Ingawa sabato hizo [saba] za kivuli zilikuwa haziwafungi tena watu, baadhi ya waumini wa Kiyahudi waliendelea kuziadhimisha [kuzitunza] siku hizo "takatifu" za Kiyahudi za kila mwaka. Hata baada ya kuongoka kwake, Paulo mwenyewe alihudhuria baadhi ya sikukuu hizo (Matendo 18:21).

Waumini wa Mataifa hawakuzijali sana "siku takatifu" hizo za Sheria ya Kafara [au Sheria ya Musa]. Hivyo siku hizo maalum kwa Wayahudi zikawa sababu ya mafarakano na machafuko ndani ya Kanisa. Katika Warumi 14 Paulo aliandika kwamba waumini hawakupaswa kuhukumiana kuhusu uadhimishaji wa siku hizo maalum za kivuli. Alikuwa haizungumzii siku ya saba ya kila juma [ambayo imo katika Amri Kumi].

Endapo Wakristo wale wa Kiyahudi wangependa kuendelea kuiadhimisha "sabato ya kivuli" ya Pasaka, "sabato ya kivuli" ya Pentekoste, na kadhalika, basi, haikuwapasa kuyashurutisha

mazoea yao juu ya waumini wale wa Mataifa. Na kwa upande mwingine, waumini wale wa Mataifa hawakutakiwa kuwahukumu waumini wale wa Kiyahudi kwa kuendelea kuziadhimisha [siku hizo].

Kusudi la Paulo katika Warumi 14 ni lile lile lililotolewa katika Wakolosai 2:14-17, ambako anasema kwamba Sheria ile ya Kafara [sio Amri Kumi] iligongomewa msalabani. Kwa kuyazingatia hayo aliwashauri waumini wa Mataifa kutomruhusu mtu ye yote kuwahukumu kwa kutokutoa sadaka za vyakula na vinywaji [Hesabu 28:1-8], kutokuziadhimisha sikukuu zile, mwezi mpya, na siku zile saba za Sabato za kivuli [zilizotajwa katika Law. 23:4-38].

Je! Inaleta Tofauti Yo yote Kuhusu Nani Tunayemwabudu?

Paulo asema kwamba watu wale wa Mataifa walipoiweka miungu ile ya uongo mahali pa Mungu pekee wa Kweli, waliibadili kweli ya Mungu [Yohana 17:17; Zaburi 119:142; Kum. 4:2] kuwa uongo. Vile vile, wanadamu walipoweka utunzaji wa siku ya kwanza mahali pa ule wa siku ya saba, waliibadili kweli hiyo ya Mungu kuwa uongo, ingawa wao wenyewe huenda wakawa hawalifahamu jambo hilo.

Iwapo watu hao walio waaminifu wangukuwa wametambua jambo linalohusika katika kuiweka kando siku ya saba na kuipendelea Jumapili, basi, wasingalithubutu kufanya kitendo hicho. Jambo linalohusika ni uasi kwake [kuvunja Amri Kumi za] Bwana [Yehova] Yesu Kristo, yaani, kuiweka kando ishara yake Kristo inayomtambulisha yeye kama Muumbaji na Mwokozi pekee, na kuikataa mamlaka yake kama Mtoa-Sheria [Mtoa-Amri Kumi].

Kama Sabato ingehusu tu pumziko la kimwili, basi, mwanadamu angeweza kuchagua siku yo yote [ya kupumzika kimwili]. Lakini hakuna hata mmoja awezaye kuitunza Sabato kikweli kweli isipokuwa kama anaingia katika pumziko lile la kiroho la Bwana. Na hilo huja tu kutokana na uzoefu wa maisha ya kila mtu katika kuipokea haki [yake Kristo] kwa njia ya imani.

Kila Sabato tunavuta pumzi mpya ya Edeni ile ilipokuwa haina dhambi, na mpya kama uumbaji ulivyokuwa. Ndani ya hiyo pia tunaionja Edeni ile itakayorejeshwa katika nchi ile mpya ambamo dhambi, magonjwa, na huzuni vitafutiliwa mbali milele.

Sabato ni kweli kwamba inatoa pumziko la kimwili kutokana na shughuli nyingi za siku zile [sita] za kazi; lakini kimsingi ipo kwa ajili ya kuburudishwa na kufanywa upya kiroho.

Furaha kamili ya Sabato ile ya kwanza kule Edeni itapatikana tena kwa watu wa Mungu waliokombolewa katika nchi mpya ijayo. Sabato hata Sabato watu wake Kristo waliokombolewa watakuja Yerusalemu Mpya kuabudu [Isaya 66:22,23].

Lakini kwa sasa, tungali bado tunaishi katika ulimwengu wa njaa, taabu, na huzuni. Kwa nini wewe usianze leo kujipatia tena furaha inayokuja kwa njia ya utunzaji sahihi wa Sabato

hiyo? Pasipo sabato, maisha yanachosha sana, ni usumbufu unaokinaisha.

SURA YA 8

Maswali Yako Yanajibiwa

=====
===

Baadhi ya maswali yanajibiwa hapa kwa msingi wa vigezo hivi: 1. Biblia ina jibu sahihi kwa kila swali linalohusu wokovu. 2. Kweli ni kitu kimoja [inapatana kabisa] na yeye aliye Kweli.

3. Biblia, ikifahamika vizuri, haijipingi yenyewe.

Swali la 1: Mungu alisema katika Kutoka 31:16,17 kwamba Sabato ni ishara kati yake na wana wa Israeli milele. Je! Sabato ilifanyika kwa ajili ya Wayahudi tu?

Bwana anathibitisha kwamba Sabato ni ishara kwa sababu aliifanya dunia hii kwa siku sita na kustarehe [kupumzika] siku ile ya saba. Uumbaji ulitokea miaka 2,000 kabla ya kuwako Myahudi wa kwanza [duniani].

Mungu aliwakabidhi Wayahudi Amri zake Kumi [ikiwamo Amri hiyo ya Sabato] pamoja na Mwana wake kwa sababu wao walipaswa kuipeleka nuru yake ulimwenguni kote. Utunzaji wa siku ya saba haujafungwa kwa Wayahudi tu kama vile Kristo (aliyezaliwa akiwa Myahudi) asivyofungwa kwa Wayahudi tu. Vitabu vyote vya Biblia viliandikwa na Waebrania. Je! viliandikwa kwa Waebrania hao tu? Biblia inasema kwamba Mungu ni Mungu wa Israeli. Je! hiyo inamaanisha kwamba yeye ni Mungu wa Israeli tu?

Agano Jipya linaonyesha kwamba tangu kusulibiwa kwake Kristo, "Israeli" wa Mungu ndani yake ina Wamataifa waliozaliwa mara ya pili au Wayahudi (Wagalatia 3:29 [Rum.2:28,29; 9:1-8]).

Majina ya makabila kumi na mbili ya Israeli ya Kiroho yameandikwa juu ya milango ile kumi na miwili ya Yerusalemu Mpya (Ufunuo 21:12). Israeli ya Kiroho, ambayo ndani yake wamo watu wote waliozaliwa mara ya pili [Wayahudi na Wamataifa] huendelea kuwako kupita ulimwengu huu na kuingia katika umilele ule. Hivyo Sabato, ishara kati ya Mungu na Israeli ya Kiroho, itaendelea milele katika nchi mpya ya Mungu (Isaya 66:22,23).

Swali la 2: Tukiyazingatia mabadiliko yaliyofanywa na wanadamu katika Kalenda, mtu ye yote anawezaje kuwa na hakika kwamba siku ya saba ni Jumamosi?

Sabato ya siku ya saba aliyoitunza Yesu alipoishi hapa ilitokea katika siku ile ya Sarateni (Saturday) kama ilivyohesabiwa na Warumi. Siku ya Sarateni, siku ya saba ya juma, imetujia sisi mpaka leo hii kama siku ya Jumamosi katika mzunguko wa juma unaoendelea [toka Edeni].

Mabadiliko katika Kalenda hayajaathiri mpangilio wa siku za juma katika mzunguko huo wa juma. Siku ya mwisho ya juma,

yaani, siku ya saba, iko mahali pale pale ilipokuwa tangu Yesu alipoitunza.

Sehemu kubwa ya ulimwengu inaukubali ukweli kwamba Kristo alisulibiwa siku ile tunayoiita Ijumaa, na kufufuka toka kwa wafu siku ile tunayoiita Jumapili. Marko 16:1,2 husema kwamba Sabato ilipokwisha kupita wanawake walikwenda kwenye kaburi lake Kristo mapema siku ile ya kwanza ya juma. Marko 15:42 huitambulisha siku ile aliyosulibiwa Kristo kuwa ni siku iliyo kabla ya Sabato.

Siku ile iliyo katikati ya Ijumaa ile ya kusulibiwa kwake na Jumapili ya kufufuka kwake, wafuasi wale wa Kristo [Wakristo waanzilishi] "walistarehe kama ilivyoamriwa [kulingana na ile amri]" Luka 23:57, KJV.

Swali la 3: Wakolosai 2:14-17 husema hivi: "Akiisha kuifuta ile hati iliyoandikwa ya kutushitaki kwa hukumu zake, iliyokuwa na uadui kwetu; akaiondoa isiwepe tena, akaigongomea msalabani; akiisha kuzivua enzi na mamlaka, na kuzifanya kuwa mkogo kwa ujasiri, akizishangilia katika msalaba huo. Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato; mambo hayo ni kivuli cha mambo yajayo; bali mwili ni wa Kristo." Je! maneno hayo yanaonyesha kwamba Sabato hiyo [ya siku ya saba] ilikuwa sehemu ya mfumo ule uliokoma pale msalabani wa maadhimisho ya Kiyahudi yaliyoambatana na dhabihu?

Kama ilivyo katika Warumi 14:5,6, Sabato zilizotajwa hapa zinahusu Sabato zile saba [za kivuli] za kila mwaka za Sheria ile ya Kafara [Ceremonial Law], ambayo iligongomewa pale msalabani. Sabato ya siku ya saba inayokuja kila juma inaendelea hata baada ya msalaba huo, kama zinavyoendelea amri zile nyingine tisa za milele za Amri Kumi za Mungu [Kut. 20:3-17].

Siku ya saba ilitengwa kwa ajili ya mwanadamu kabla hajatenda dhambi. Kwa ajili hiyo isingeweza kuwekwa pamoja na "Sabato zile" ambazo Paulo alizitangaza kuwa zilikuwa kivuli cha kazi yake Kristo ya kumtakasa na kumkomboa mwanadamu toka dhambini. Kwa hiyo, katika Wakolosai 2:14-17 Paulo alikuwa hatetei kuifutilia mbali Sabato hiyo [ya siku ya saba], wala zile Amri Kumi.

Swali la 4: Utunzaji wa siku ya saba unafungamana na Agano la Kale ambalo mahali pake pamechukuliwa na Agano Jipya ambalo sisi tunaishi chini yake, au sivyo?

Katika Waebrania 8:8-10 Paulo analitangaza Agano Jipya akinukuu maneno haya kutoka katika Yeramia 31:31-34.

"Nita...fanya agano jipya na nyumba ya Israeli, na nyumba ya Yuda.... Bali agano hili ndilo nitakalofanya na nyumba ya Israeli, baada ya siku zile, asema BWANA; Nitatia sheria yangu [Amri Kumi] ndani yao, na katika mioyo yao nitaiandika; nami

nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu."

Chini ya Agano Jipya, Mungu hasemi, Nitawapa ninyi sheria mpya iliyo tofauti na hii. Wala hasemi, Nitaisahihisha sheria yangu ili iwe nzuri zaidi, na kuwapa ninyi siku mpya takatifu ya kila juma ili mpate kuitunza.

Anaonyesha kwamba juu ya mioyo ya watu wale walioongoka, ataiandika sheria yake ile ile ya Amri Kumi ambayo zamani alikuwa ameiandika juu ya mbaio mbili za mawe [Kut. 20:3-17].

Kristo ni Muumbaji na Mwokozi chini ya maagano yote mawili, la zamani na lile jipya. Nayoy [Sabato] inaendelea katika vizazi vyote kama ishara ya milele ya Muumbaji-Mkombozi yule yule mmoja (Isaya 66:22,23).

Swali la 5: Je, hivi mtume Yohana katika Ufunuo 1:10 anaitaja Jumapili kama ndiyo Siku ya Bwana?

Yohana asema, "Nalikuwa katika Roho, Siku ya Bwana." Yeye hapo hataji siku gani ya juma kuwa ndiyo Siku ya Bwana. Katika suala hili yatupasa kulinganisha Maandiko kwa Maandiko, na kuliacha Neno la Mungu lipate kutufafanulia siku gani kuwa ndiyo Siku ya Bwana.

Siku ya Bwana ni siku ile ambayo Kristo ndiye Bwana wake. Yeye anatangaza kwamba ndiye Bwana wa Siku ya Sabato (Marko 2:28). Hivyo Sabato yake Kristo inapaswa kuwa ndiyo Siku ya Bwana. Wale wanaotangaza kwamba katika Maandiko Sabato na Siku ya Bwana ni siku mbili tofauti wanaweka tofauti mahali ambapo hakuna tofauti yo yote.

Swali la 6: Je, watu wale walio waaminifu wanaoitunza Jumapili watapotea?

Haki yake Kristo huzifunika dhambi zile zinazotendwa kwa ujinga [kutokujua - Matendo 17:30,31]. Hakuna wanaohukumiwa adhabu isipokuwa kama wao wanaiielewa ile kweli, lakini kwa makusudi kabisa wanakataa kuitii. Neno lasema hivi, "Maana, kama tukifanya dhambi kusudi [kwa makusudi] baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi [damu ya Yesu haiwezi tena kutusafisha dhambi zetu]." Waebrania 10:26.

Mtu anapojua kile kilicho chema, kisha akapuuzia kukifanya, kwake hicho ni dhambi (Yakobo 4:17). Yesu alifafanua tofauti iliyopo kati ya mtu yule asiyeijua kweli na yule anayekataa kuitii kweli ile anayoiujua. "Yesu akawaambia, Kama mngekuwa vipofu, msingekuwa na dhambi; lakini sasa mwasema, Twaona; basi dhambi yenu yakaa" Yohana 9:41.

Njia pekee iliyo salama ni kuitii upesi ile kweli kadiri inavyokujia kutoka katika Neno la Mungu. Tunapofanya hivyo, damu yake Kristo inaendelea daima kutusafisha na dhambi yote. Hivyo twasoma maneno haya: "Bali tukienda nuruni [Mit.6:23; Zab.119:130],... damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote" 1 Yohana 1:7. (Angalia Yohana 8:47; Luka 8:15.) Mungu

anamwagalia kila mtu aliye mwaminifu, na kwa njia yake mwenyewe atafanya kazi ya kumfundisha kweli halisi kila mmoja aliye hivyo.

Swali la 7: Ni nani aliyeibadili Sabato kutoka siku ya saba, au Jumamosi, kwenda siku ya kwanza ya juma, au Jumapili? Na badiliko hilo lilitokea lini?

Hakuna tarehe moja maalum inayoweza kutolewa, kwa vile badiliko hilo lilitokea polepole kuanzia karibu na mwaka ule wa 150 hadi mwaka wa 400 Baada ya Kristo.

Kwa kawaida Wakristo hawakujizua kufanya kazi zao za kawaida siku ile ya Jumapili mpaka hapo amri ya kwanza ya Jumapili inayojulikana ilipotolewa na Konstantino katika mwaka ule wa 321. Baraza la Kanisa [Katoliki] lililofanyika Laodikia baadaye kidogo lilitoa amri kwamba Wakristo ni lazima waache kupumzika siku ya Jumamosi, na tena, kwamba ni lazima kuitunza Jumapili kama Sabato.

Unabii wa Danieli ulionyesha kwamba mamlaka ile iliyounganisha dini na serikali [chini ya mtawala mmoja] ingeazimu [ingefikiria] kubadili majira na sheria ya Mungu [Amri Kumi] (Danieli 7:25).

Katika baadhi ya hati zake rasmi, Kanisa Katoliki linatangaza kwamba ndilo lililoibadili Sabato kutoka Jumamosi kwenda Jumapili.

Ensaiklopedia ya Kikatoliki yasema hivi:

"Kanisa [Katoliki]... baada ya kubadili siku ya mapumziko kutoka Sabato ile ya Kiyahudi, au siku ya saba ya juma, kwenda siku ile ya kwanza, likaifanya amri ile ya tatu [ya nne, wamefuta ya pili] kuitaja Jumapili kama ndiyo siku inayopaswa kutakaswa kama Siku ya Bwana." Gombo la 4, uk. 153, Toleo la 1913.

Katika Katekisimu ya Kikatoliki inayojulikana sana twasoma maneno haya:

"Swali: Siku gani ni siku ya Sabato?

"Jibu: Jumamosi ndiyo Siku ya Sabato.

"Swali: Kwa nini sisi tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi?

"Jibu: Tunaitunza Jumapili badala ya Jumamosi kwa sababu Kanisa Katoliki, katika Baraza lake la Laodikia [lililofanyika karibu na mwaka 336 B.K.], lilihamisha ibada kutoka Jumamosi kwenda Jumapili." ----- Peter Geiermann, katika The Convert's Catechism of Catholic Doctrine, Toleo la 1936, uk. 50.

Swali la 8: Kwa vile Biblia inaonyesha wazi kuwa siku ya saba ndiyo siku sahihi ya kuitunza kama Sabato, mbona karibu wote huitunza siku ya kwanza, Jumapili?

Katika 2 Wathesalonike 2 Paulo aliandika kwamba "ukengeufu" [kuiacha njia ya kweli] ungetokea, tena anaongeza kusema kwamba "siri ya kuasi hivi sasa inatenda kazi." Katika karne zile za mwanzo zilizofuata baada ya kufa mitume wote, kanisa lilijifungamanisha sana na ulimwengu kiasi kwamba desturi zisizopatana na Maandiko ziliingizwa ndani yake kutoka katika dini za kipagani. Miongoni mwa hizo ni desturi ile ya kuabudu katika siku ile ya jua (Sun-day) ili kuadhimisha ufufuo wa Yesu, ambao ulitokea pia Jumapili. Kwa karne kadhaa siku zote mbili, ya saba na ya kwanza, zilitunzwa. Lakini polepole siku ile ya kwanza ikaisukumia nje ile ya saba.

Utunzaji wa siku ya Jumapili hauna mamlaka [idhini] yo yote kama vile yalivyo yale matumizi ya maji matakatifu, tohara [purgatory], maungamo kwa kasisi [padre], uadhimishaji wa Kwaresima, Jumatano ya Majivu, ibada ya Maria, na kadhalika. Hakuna idhini ya Biblia kwa jambo lo lote kati ya hayo.

Mbona, basi, Waprotestanti wanaitunza Jumapili? Kizazi cha sasa kinaitunza Jumapili kwa sababu wazazi wao waliowatangulia waliitunza Jumapili. Waprotestanti wale wa kwanza walipoliacha Kanisa Katoliki walihama na utunzaji wa Jumapili pamoja nao. Ingawa Waprotestanti walisaidia kubadilisha desturi nyingi potofu, walishindwa kufanya badiliko hilo moja.

Swali la 9: Kama siku ya saba bado inaendelea kuwa Sabato ya kweli, kwa nini amri zote Kumi zimerudiwa katika Agano Jipya kasoro amri ile ya Sabato?

Ni amri tatu tu katika zile Amri Kumi ambazo zimerudiwa neno kwa neno katika Agano Jipya ----- ya sita, ya saba, na ya nane [Kutoka 20:13-15]. Hii haimanishi kwamba zile nyingine saba haziwafungi watu. Hapakuwa na haja yo yote kwa amri hizo kurudiwa wala kutungwa upya katika Agano Jipya.

Sheria inapotungwa kwa mara ya kwanza, huendelea kuwafunga watu mpaka hapo itakapofutwa [itakapobatilishwa], au itakapokoma kutokana na mipaka yake iliyowekewa, au itakapoyapoteza mamlaka yale yaliyo nyuma yake [yaliyoitunga]. Hakuna kitu cho chote katika Agano Jipya kinachotuonyesha kwamba sehemu yo yote ya Amri zile Kumi imefutwa, au imekoma kutokana na ufinyu wa mipaka yake, au imeipoteza Mamlaka [Mtoa-Sheria] iliyo nyuma yake. Agano Jipya linaziangalia Amri zote Kumi kuwa zinawafunga watu wote katika siku zile za Mitume (Yakobo 2:8-12; 1 Yohana 3:4; Waefeso 6:2; Warumi 3:31; 7:7,12; 13:8-10). Kwa hiyo Sabato ya siku ya saba inaendelea kuwapo.

Agano Jipya linaitaja amri ile ya Sabato kuwa ni siku iliyofuata baada ya siku ile ya Kusulibiwa kwake Kristo (Luka 23:56). Ukweli ule kwamba ni Kristo mwenyewe aliyezitangaza Amri Kumi kutoka mbinguni pale Sinai huonyesha kwamba ile ya nne ni amri itokayo kwake Kristo ambayo inawataka watu wote kuitunza siku ile ya saba.

Agano Jipya linaitaja Sabato ya siku ya saba zaidi ya mara hamsini, lakini hakuna mahali po pote inapoikataa au inapopendekeza siku nyingine kuchukua mahali pake. Kama ingekuwa imeikataa Sabato hiyo ya siku ya saba, basi, kuikataa huko kungekuwa sawa na kumkataa Kristo kuwa siye Muumbaji wala Mtakasaji. Kwa kuitetea Sheria ile ile ya haki [Amri Kumi], injili ile ile, Mwokozi yule yule, na Sabato ile ile kama Agano la Kale lifanyavyo, Agano Jipya huonyesha kwa mfano umoja wa kweli yote ndani yake Kristo.

Kristo alitabiri juu ya kuharibiwa kwa hekalu na mji ule wa Yerusalemu, akiwaonya wanafunzi wake kukimbia wakati majeshi ya adui yatakapoikaribia Yudea. Unabii huo ulitimia miaka kama thelathini na tisa hivi baadaye, yaani, katika mwaka ule wa 70 B.K. "Ombeni, ili kukimbia kwenu kusiwe wakati wa baridi, wala siku ya Sabato" Mathayo 24:20. Sabato ya siku ya saba ile ile ambayo wanafunzi wake walikuwa wanaitunza wakati ule ingekuwa bado ndiyo Sabato ya Bwana mwaka ule wa 70 B.K., yaani, miaka thelathini na tisa baada ya ufufuo wake.

Kitabu cha Matendo ya Mitume katika kipindi cha karibu miaka thelathini hivi baada ya ufufuo kinaitaja siku ya saba kuwa ndiyo Sabato peke yake iliyojulikana miongoni mwa Wakristo wale wa kwanza (Matendo 13:14,27,42-44; 15:21; 16:13; 17:1-3; 18:4).

(1) Siku ya saba peke yake ndiyo siku aliyopata kuitakasa Kristo Muumbaji, au kuitenga kwa ajili ya mwanadamu. (2) Siku ya saba peke yake ndiyo siku aliyopata kuibariki Mwana wa Mungu, au kuitakasa, kwa ajili ya mwanadamu. (3) Siku ya saba ya juma ni siku pekee ambayo Kristo kama Bwana [Yehova) wa Amri Kumi aliyopata kumwamuru mwanadamu awaye yote kuitunza. (4) Siku ya saba ni siku ya pekee aliyoiweka Bwana Yesu Kristo kuwa ishara yake inayoonyesha kwamba yeye ni Muumbaji ----- yaani, Mungu na Mwokozi peke yake. (5) Siku ya saba peke yake ndiyo inayoadhimisha uumbaji, na kuumbwa-upya katika wokovu.

Mimi nililelewa nikiwa naitunza Jumapili. Niliitunza kwa makini sana, kwa sababu nilidhani ilikuwa siku takatifu ya Bwana. Lakini katika nuru ya ushahidi wa Maandiko iliyotolewa hapo juu, sikuwa na jingine lolote la kufanya bali kuchagua kwenda katika nuru aliyokuwa ameipeleka Mungu. Kwa hiyo nikaamua kugeuka na kuiacha Sabato-ya-Jumapili iliyowekwa-na-mwanadamu na kuanza kuitunza Sabato ya kweli ya Kristo. Na katika miaka yote iliyopita hadi sasa uamuzi wangu huo umeniletea thawabu kubwa mno na mibaraka.

Kurejeshwa Kwa Sabato Mahali Pake Kulitabiriwa

=====
===

Paulo alitabiri kwamba baada ya kufa kwake waalimu wa uongo wangeinuka [wangetokea] kanisani ambao wangeyachanganya mafundisho potofu pamoja na kweli zile za Ukristo (Matendo 20:29,30; 2 Wathesalonike 2:3-5).

Mitume wale walipokufa, wengi ndani ya kanisa walianza kuyasahau mafundisho ya Yesu na yale ya mitume. Taratibu za ibada, ibada yenyewe, na desturi ambazo Yesu wala mitume wake hawakupata kuzifundisha kamwe zikaingia [kanisani] na kuanza kutumika. Mojawapo ya hizo ni kule kuiheshimu Jumapili kwa kukumbuka [kuadhimisha] ufufuo wake Kristo.

Mwanzoni wengine walianza kukusanyika pamoja jua lilipokuwa linachomoza siku ile ya Jumapili kwa ibada fupi kabla ya kwenda kufanya kazi zao za kawaida. Lakini kadiri karne nyingi zilivyozidi kupita ndivyo Jumapili ilivyoanza na kuendelea zaidi na zaidi kuchukua sura ya siku ya mapumziko zaidi na zaidi, ijapokuwa kwa wakati uo huo wengi walikuwa bado wanaitunza Sabato ya siku ya saba. Siku zote mbili zikawa zinatunzwa kwa pamoja moja baada ya nyingine. Polepole, kwa watu wengi, Jumapili ikaanza kuisukumia kando Jumamosi na kuwa kama siku ya mapumziko na ibada. Hiyo ilitokana na mambo haya kadhaa:

Watu wengine kule Roma na mahali pengine wakaanza kufunga [kuacha kula chakula] siku ya Sabato, labda ili kujitofautisha na Wayahudi ambao pia waliitunza siku ya saba ila hawakufunga siku ile. Jambo hilo kwa kawaida likaifanya siku hiyo isipendwe na watu wengi hasa miongoni mwa vijana. Pia, wengi miongoni mwa

wale waliokuwa wapagani zamani, ambao katika ibada yao ya kuliabudu jua walikuwa wameiheshimu siku hiyo ya jua (Sunday), walipoingia katika mikusanyiko ya Kikristo, walikuwa na mwelekeo wa kuja pamoja na kuendelea na mazoea yao ya kuitunza siku hiyo ya kwanza kama sikukuu ya kidini.

Katika karne ile ya nne Mfalme Konstantino alitoa amri ya Jumapili, na muda mfupi baadaye Baraza la Kanisa [Katoliki] la Laodikia likaukubali mwelekeo huo wa kimagharibi uliokengeuka kutoka katika siku ya saba na kwenda katika siku ya kwanza kwa kupiga kura ya kuihamisha ibada hiyo. Kuanzia hapo na kuendelea mapokeo yakawa karibu yameuzika kabisa utunzaji sahihi wa Sabato [Jumamosi].

Sabato ya Kweli Sikuzote Iliendelea Kutunzwa Na Watu Fulani

Walakini, jambo hilo lilikuwa ni kweli tu katika Roma na Aleksandria [Misri] katika karne zile za mwanzo. Mwanahistoria Socrates Scholasticus, akiandika karibu na mwaka ule wa 450 B.K. anasema hivi: "Ingawa karibu makanisa yote ulimwenguni kote yanaadhimisha meza ya Bwana katika siku ya Sabato (yaani, siku ya saba) ya juma, hata hivyo, Wakristo walioko Aleksandria na kule Roma, kutokana na mapokeo fulani ya zamani wameacha kabisa kufanya hivyo." Ecclesiastical History, Kitabu cha 5, Sura ya 22.

Wakristo katika nchi ile ya Waskoti (Scotland) waliitunza Sabato ya siku ya saba mpaka wakati ule wa Malkia Margaret karibu miaka elfu moja baada ya Mitume. Na Wakristo wale wa Ethiopia waliitunza Sabato mpaka wamishonari wa Kijesuti [Chama cha Yesu] walipofika na kuwazuia katika karne ile ya 17. Katika Ghana ya zamani watu wa kabila la Akani waliiangalia Jumamosi kama siku ya pekee, Memeneda, maana yake "Siku ya Mungu." Waghana wanawaita Wazungu "Kwasi Groni" kwa sababu wamishonari hao weupe waliwafundisha kuitunza Jumapili.

Walakini, Maandiko yalitabiri sio tu ukengeufu huo ulioenea kote kutoka katika ile kweli, bali pia kurejeshwa kwa kweli zote zilizokuwa zimezikwa chini ya mapokeo ya wanadamu wakati ule wa uasi mkuu [wa kanisa].

Kitabu cha Ufunuo kinakiunga mkono kitabu cha Danieli na kutoa mwanga wa ziada juu ya jambo hilo. Ufunuo 11:3-12 hutabiri ushindi wa ile kweli chini ya mfano wa mashahidi wawili wa Mungu, yaani, Agano la Kale na Agano Jipya. Mungu angewafanya mashahidi hao wawili ku"toa unabii siku elfu na mia mbili na sitini, hali wamevikwa magunia" Ufunuo 11:3. Tukitumia kanuni ya unabii ya siku moja-mwaka mmoja (Danieli 9:20-27; Ezekieli 4:6; Hesabu 14:34), tunagundua kwamba siku hizo 1,260 huwakilisha miaka 1,260. Siku zote [katika kipindi hicho] palikuwa na wachache waliokuwa wakiitunza Sabato!

Tangu mwanzo wa kipindi hicho cha siku-miaka 1,260 mpaka kufikia kwenye Matengenezo ya Kanisa yaliyofanywa na Waprotestanti katika karne ile ya kumi na sita, wale waliojidai kuwa ni watunzaji wa Neno la Mungu waliizuia Biblia wasiisome watu. Lakini nuru ya ile kweli ikaanza kuingia ulimwenguni wakati wa kuja kwao wale Wanamatengenezo ya Kanisa kama vile Martin Luther. Unabii huo wa mashahidi wawili huonyesha kwamba kweli ya Neno la Mungu ingeanza kwa mwanga mkali zaidi baada ya kumalizika miaka ile 1,260 ya [Zama zile za] Giza. Na ndivyo ilivyozidi kuangaza zaidi.

Unabii wa Ufunuo 12 pia hutoa mwanangaza huo. Biblia inaliwakilisha Kanisa la Mungu la kweli kama mwanamke safi [bikira] (Ufunuo 12:1; Yeremia 6:2,KJV). Kanisa hili la kweli lilikuwa limefichwa katika hali ya upweke katika kipindi hicho chote cha siku-miaka 1,260 kuanzia mwaka 538 mpaka 1798 B.K. (Ufunuo 12:14,16,6). Lakini katika kipindi chake cha mwisho Kanisa hilo linaongozwa na "Waliosalia" [au Wamasalio] hao "wazishikao amri [kumi] za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu" Ufunuo 12:17.

Hivyo kuna kazi ya kuirejesha mahali pake Sabato ya kweli ya Kristo inayofanywa na Kanisa lake la Kweli katika kipindi hiki cha mwisho kabla Kristo hajaja tena.

Inaonekana wazi ya kuwa injili ya kweli, Sabato ya kweli, na imani ya kweli vitaonekana katika kanisa hilo la kweli la Mungu. [Kanisa] hilo ndilo "nguzo na msingi wa kweli."

1 Timotheo 3:15.

Ujumbe Wa Mungu Wa Siku za Mwisho

Kwa mfano wa malaika wale watatu wanaohubiri injili ya kweli kwa kila mtu tunagundua ni akina nani waliomo katika hao Wamasalio:

"Kisha nikaona malaika mwingine, akiruka katikati ya mbingu, mwenye injili ya milele, awahubiri hao wakaa juu ya nchi, na kila taifa na kabila na lugha na jamaa, akasema kwa sauti kuu, Mcheni Mungu, na kumtukuza kwa maana saa ya hukumu yake imekuja. Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi na bahari na chemchemi za maji. Kisha mwingine, malaika wa pili, akafuata, akisema, Umeanguka, umeanguka Babeli, mji ule ulio mkubwa, maana ndio uliowanyweshwa mataifa yote mvinyo ya ghadhabu ya uasherati wake. Na mwingine, malaika wa tatu, akawafuata, akisema kwa sauti kuu, Mtu awaye yote akimsujudu huyo mnyama na sanamu yake, na kuipokea chapa katika kipaji cha uso wake, au katika mkono wake, yeye naye atakunywa katika mvinyo ya ghadhabu ya Mungu iliyotengenezwa, pasipo kuchanganywa na maji, katika kikombe cha hasira yake; naye atateswa kwa moto na kiberiti mbele ya malaika watakatifu, na mbele za Mwana-Kondoo" (Ufunuo 14:6-10).

Kwa vile kuihubiri injili hiyo wamekabidhiwa wanaume na wanawake na sio malaika, basi, malaika hao watatu huliwakilisha kundi la wanaume na wanawake watakaozitangaza kweli hizo kwa ulimwengu wote. Wale wanaoupokea ujumbe huo wa aina tatu uliotoka mbinguni watabainishwa na watu wengine wote kwa kuzishika amri [kumi] za Mungu na imani ya Yesu. Hapa ndipo upo ule utabiri kuhusu mkazo utakaowekwa juu ya amri zote [kumi], ikiwamo ile ya Sabato: "Hapa ndipo penye subira ya watakatifu, hao wazishikao amri [kumi] za Mungu, na imani ya Yesu," fungu la 12.

Amri [Kumi] za Mungu na imani ya Yesu hutoa muhtasari wa kila kitu ambacho mtu awaye yote anahitaji ili kuishi maisha ya haki na kwa furaha, kwa maana wale walio na imani ya Yesu hawatataka tu kuzishika amri [kumi] za Mungu bali watapokea pia uwezo wa kufanya hivyo kwa njia ya imani katika Yesu Kristo.

Wengine wanadai kwamba imani katika Yesu inamwachilia mtu huru mbali na utii. Lakini imani ya kweli katika Yesu inajionyesha yenyewe kwa njia ya utii kwa amri zake [kumi]: "Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake [kumi]. 1 Yohana 2:3. Kwa njia ya imani, Kristo huishi maisha yake yale ya utii ndani ya muumini. Hivyo imani ya Yesu na kuzishika zile amri [kumi] vimeunganishwa pamoja, wala haviwezi kutenganishwa kamwe kama vile zilivyo sura mbili [pande mbili] za sarafu.

Baada ya ujumbe huo wa aina tatu kuwakusanya pamoja watu wale waliojiweka tayari kwa ajili ya Bwana, hatua inayofuata katika mpango wa Mungu imewekwa katika fungu lile la 14,15.

"Kisha nikaona, na tazama, wingu jeupe, na juu ya wingu hilo ameketi mmoja, mfano wa Mwanadamu [Kristo], mwenye taji ya dhahabu juu ya kichwa chake, na katika mkono wake mundu mkali. Na malaika mwingine akatoka katika hekalu, akimlilia kwa sauti kuu yeye aliyekuwa ameketi juu ya lile wingu, Tia mundu wako, ukavune; kwa kuwa saa ya kuvuna imekuja; kwa kuwa mavuno ya nchi yamekomaa" Ufunuo 14:14,15.

Kuja Kwa Kristo Mara ya Pili

Mafungu hayo yanahusu kuja kwa Kristo mara ya pili kuvuna mavuno ya ujumbe ule wa injili. Ujumbe huo wa aina tatu utatayarisha njia kama vile ujumbe ule wa Yohana Mbatizaji ulivyotayarisha njia kwa kuja kwake Kristo mara ya kwanza.

Hivyo ujumbe huo wa aina tatu ni awamu ya mwisho ya kuihubiri injili ile moja ya kweli kwa vizazi vyote. Ujumbe huo ni mwaliko wa Kristo uliotolewa kwetu kwa moyo wa upendo ili tupate kuupokea wokovu wake. Tena ishara hizo alizoziweka Mungu zinaonyesha kwamba kuja kwake Kristo kunakaribia sana, pia zinaonyesha kwamba ujumbe huo wa aina tatu ndio ujumbe aliouchagua Mungu kwa wakati huu.

Ujumbe huo wa aina tatu una zaidi ya hizo kweli zilizotajwa na malaika hao watatu. Kwa kuwa ujumbe huo unaitwa "injili ya milele" (Ufunuo 14:6), basi, ndani yake una kweli zote za injili ambazo zimesahauliwa kwa nyakati zilizopita.

Mambo matatu katika ujumbe huo (Ufunuo 14:6-12) huonyesha kwamba Sabato ya kweli ya Kristo itarejeshwa mahali pake pa halali katika harakati za kuitangaza injili hiyo:

(1) Ujumbe huo uliotumwa kutoka mbinguni unatutaka sisi ku"msujudi[a] yeye aliyezifanya mbingu na nchi" Ufunuo 14:7. Kwa kuwa, kama tulivyokwisha kuona, Bwana Yesu Kristo ndiye Yule aliyezifanya mbingu na nchi, basi, kifungu hicho cha maneno kinatutaka sisi kumheshimu Kristo kama Muumbaji wetu katika wakati huu ambapo mamilionni karibu wamemsahau kabisa kuwa ndiye Muumbaji!

Ni Kristo mwenyewe aliyeamuru utunzaji wa siku hiyo ya saba kama ishara ya kuonyesha kwamba sisi tunamwabudu yeye kama Muumbaji wa mbingu na nchi. Yeye, kama Muumbaji, aliifanya mbingu na nchi kwa siku sita na kustarehe [kupumzika] siku ya saba (Kutoka 20:8-11). Sabato yake ni ishara ya uweza wake wa uumbaji (Kutoka 31:17). Hivyo kwa kuitunza siku ile ya saba tunaweza kuonyesha imani yetu katika uumbaji wa dunia hii kwa siku sita uliofanywa na Mwana huyo wa Mungu. Mwito huo wa siku za mwisho usemao, "Msujudieni yeye aliyezifanya mbingu na nchi," unahusu kuirudia Sabato ile ya uumbaji.

Ujumbe ule wa malaika watatu unawaita watu katika kila nchi ambao wataitakasa siku ile ya saba kama ishara itakayoonyesha kuwa wao wanamwamini Kristo kama Muumbaji.

Kusema kweli, amri hiyo hutoa dawa inayofaa sana kwa wakati huu ili kuipinga nadharia ile potofu ya evalusheni ambayo imewafanya wengi wasiweze kukiamini kitabu kile cha Mwanzo.

(2) Katika Ufunuo 14:12 tunajifunza kwamba wale wanaoukubali na kuutangaza ujumbe huo watabainishwa kwa ukweli wa kwamba wanashika vyote viwili, amri [kumi] za Mungu na imani ya Yesu. Kwa vile mojawapo ya amri hizo [kumi] hututaka sisi kuitakasa siku ile ya saba, basi, hao wanaozishika amri zote [kumi] huitakasa siku hiyo ya saba kama Sabato.

(3) Kumwabudu Muumbaji dhidi ya kuziabudu mamlaka zile zilizoasi ndiko kutakakoleta jaribio hilo: Je! nitamtii Kristo kama mwenye mamlaka kupita wote na kuitunza siku yake ya saba kama ishara inayoonyesha kwamba yeye ndiye Bwana [Yehova], Muumbaji, na Mwokozi peke yake? Au, je! nitaitii mamlaka hiyo asi ambayo imeiweka Jumapili mahali pa Sabato ya Kristo ya siku

ya saba?

Thawabu Tukufu Kwa Utii

Iwapo mtu ataitunza Sabato kama vile Bwana anavyoamuru, hapo "ndipo utakapojifurahisha katika BWANA; nami nitakupandisha mahali pa nchi palipoinuka; nitakulisha urithi wa Yakobo baba yako; kwa maana kinywa cha BWANA kimenena hayo" Isaya 58:14.

Urithi wa Yakobo ni urithi wa babu yake, Ibrahimu, ambao ni ile Yerusalemu Mpya na Nchi Mpya ijayo (Matendo 7:3-5; Warumi 4:13; Waebrania 11:8-16). Urithi wa Yakobo ni pamoja na makao yale yenye furaha ya milele katika Yerusalemu ile ya mbinguni na katika Paradiso itakayorejeshwa katika nchi ile mpya. Ni ahadi ilioje! Ni jambo la kutia moyo lililoje kwako wewe na kwangu mimi linalotuwezesha kukata shauri la kudumu kwa kujisalimisha kabisa kwa Yesu!

Kama ishara ya uumbaji na uweza wake Mungu, Sabato inahakikisha upatikanaji wa uweza wa Mungu unaohitajika kutupatia ushindi, wokovu, utakaso, ukamilifu wa Kikristo, na uzima wa milele. Inatuhakikishia sisi ya kwamba Mungu wa milele ndiye makazi yetu na mikono yake ya milele i chini yetu (Kumbukumbu la Torati 33:27).

Sasa ndio wakati wa kuitetea Sabato ya Mungu iliyokanyagwa chini.

SURA YA 10

"Wakati Umetimia"

=====
===

Yesu alipoanza kuhubiri, alisema, "Wakati umetimia...; tubuni na kuiamini injili" Marko 1:15. Alianza kazi yake wakati ule ule hasa aliopangiwa na Mungu kama ilivyotabiriwa katika Danieli 9:24,25.

Alipotoa hotuba [mahubiri] yake ya kwanza katika mji ule wa nyumbani kwake, alisoma habari ya kazi ile atakayofanya Masihi hapo atakapokuja kutoka katika unabii wa Isaya 61:1,2. Kisha akawaambia, "Leo maandiko haya yametimia masikioni mwenu" Luka 4:16-21.

Viongozi wale wa Kiyahudi walipomwuliza Yohana Mbatizaji ya kuwa yeye alikuwa nani, aliutaja unabii (wa Isaya 40:3) uliokuwa ukitabiri ujumbe wa pekee utakaotolewa wakati Masihi alipokuwa karibu kutokea, kutengeneza njia na kuwaandaa watu wawe tayari kumpokea yeye [Masihi]. Mungu alimchagua Yohana kuutangaza ujumbe huo (Yohana 1:19-23). Naye alihubiri ujumbe sahihi kwa wakati sahihi.

Vile vile, tapo [kundi] hili la matengenezo ya Sabato limekuja katika ulimwengu wetu wa kisasa kwa kutimiza moja kwa moja [unabii wa] Ufunuo 14:6-15.

Ujumbe huo wa aina tatu unayakamilisha matengenezo hayo kutoka katika mafundisho potofu ya uasi ule mkuu, ulioiacha kweli ile ndani ya Kristo, hivyo kuikamilisha kazi ile ya injili.

Unabii Uhusuo Wakati Mrefu Sana Katika Maandiko

Unabii ule unaopatikana katika Danieli 8:12-14 unaungana na ule wa Ufunuo 14:6-14 na kuonyesha kwa usahihi mwaka ule Matengenezo ya Sabato ya siku za mwisho yatakapotokea [yatakapoanza]. Danieli anaonyesha kwamba mamlaka fulani asi ya kidini "ikaiangusha kweli (Yohana 17:17; Zaburi 119:142] hata chini" Danieli 8:12.

Kweli hiyo iliyoangushwa hivyo chini ni pamoja na Sabato ya Kristo, pamoja na kweli nyingine za injili kama vile kazi ya Kristo katika patakatifu pale pa mbinguni. Kwa kulijibu swali lile lililohusu hata lini kweli hiyo ya patakatifu na kweli hizo nyingine zingeendelea kuangushwa chini, malaika yule alisema, "Hata nyakati za jioni na asubuhi [siku] elfu mbili na mia tatu; ndipo patakatifu patakapotakaswa" Danieli 8:14.

Ujumbe huo ulionyesha kwamba matengenezo ya kweli hizo zilizosahauliwa yangukuja baada ya kumalizika kipindi hicho cha unabii cha siku au miaka 2,300. Sura ile ya tisa ya Danieli hutufunulia kwamba kipindi hicho cha siku au miaka 2,300 kina sehemu kuu mbili: majuma sabini (au kipindi cha siku au miaka 490) na sehemu iliyobaki ya kipindi cha siku au miaka 1,810 (Danieli 9:24). Unabii huo pia unaonyesha kwamba kipindi hicho cha siku au miaka 2,300 kineanza kwa tangazo lile la kuwarudishia tena uwezo wao [Wayahudi] wa kujitawala kule Yerusalemu (Danieli 9:24,26).

Historia huonyesha kwamba jambo hilo lililotokea katika kipindi kile cha majira ya kupukutisha [Septemba hadi Novemba] cha mwaka ule wa 457 K.K. Tukihesabu kwenda mbele miaka hiyo

2,300 kuanzia mwaka ule wa 457 K.K., tunagundua kwamba majira ya kupukutisha ya mwaka wa 1844 ulikuwa ndio mwisho wa hizo siku au miaka 2,300 ya Danieli 8:14. Chini ya ujumbe ule wa aina tatu uliotajwa katika Ufunuo 14:6-12, yaani, tangazo lililoenea katika ulimwengu mzima la kweli zile zilizosahaulika, ikiwamo na Sabato ya amri ya nne, ulipangwa kuanza mwaka ule wa 1844.

Kama matokeo ya kujifunza Biblia, katika mwaka ule wa 1844 kikundi cha watu karibu arobaini hivi, kiliacha kutunza Jumapili na kuanza kuitunza siku ya saba. Wengine nao wakaikubali Sabato mara moja pamoja na kweli zile nyingine za pekee za ujumbe ule wa aina tatu. Katika mwaka ule wa 1860 Wasabato hao wakachagua jina la "Waadventista Wasabato [wa siku ya saba]" ili kuwatofautisha na wengine.

Unabii huo wa Ufunuo 14:6-12 uliagiza kutangazwa kwa kweli hizo za pekee kwa kila nchi. Hivyo, kutokana na mwanzo huo mdogo sana katika mwaka ule wa 1844, wametawanyika ulimwenguni kote. Hivi sasa wako karibu milioni tano katika nchi mbalimbali [takwimu za 1998 ni milioni 10], wanaitunza Sabato ya kweli inayotangazwa katika ujumbe huo wa aina tatu.

Tapo hili [kundi hili] halijaja kwa mpango wa wanadamu, bali kwa mujibu wa mpango wa Mungu uliokusudiwa kabla yake katika unabii wa Danieli na Ufunuo. Watu hawa hawajafuata "hadithi zilizotungwa kwa werevu," bali neno lile imara la unabii wa Mungu (2 Petro 1:16-21).

Jinsi Unabii Ulivyotimizwa

Yohana Mbatizaji alionyesha utimilizo wa Isaya 40:3 katika utume wake kama ushahidi kwamba alikuwa akitangaza mwito wa Mungu kwa saa ile. Yesu alionyesha utimilizo wa Isaya 61:1,2 katika utume wake kama ushahidi kwamba yeye alikuwa ndiye yule Masihi aliyeahidiwa. Vile vile, utimilizo wa Ufunuo 14:6-12 na 12:17 katika kutokea kwao na kazi ya Waadventista Wasabato ni ushahidi kwamba kwa wakati ule ule sahihi wanautangaza ujumbe ule sahihi utokao kwa Mungu.

Unabii huo wa Ufunuo 14:6-12 unaendelea kutimizwa kwa kuibuka na kuenea ulimwenguni kote kazi ya Waadventista Wasabato. Maamuzi fulani ya maana yanayohitimisha suala hili ni haya: (1) Wao si kanisa au dhehebu tu jingine, bali wanatimiza unabii uliowekwa na Mungu wa tapo [kundi] hilo litakalotengeneza njia tayari kwa marejeo yake Kristo; (2) wao ndio wanaounda jumua ya watu wa Mungu waliosalia [Wamasalio] kwa siku hizi za mwisho, ambao [Mungu] anataka kila mtu achague kusimama pamoja nao; (3) hizo ndizo kweli muhimu ambazo Mungu amezichagua ili zipate kuhubiriwa, kusadikiwa, na kutiiwa katika siku hizi zetu; (4) tapo [kundi] hili la Waadventista lina mwisho mtukufu utakaotokea atakapokuja Bwana.

Katika maono Yohana aliliona kundi la watu wa Mungu

linalomtii likisimama juu ya bahari ya kioo mbele ya kiti cha enzi cha Mungu mbinguni, baada ya kuja kwa Kristo juu ya wingu (Ufunuo 15:2,3). Hao ndio "wale wenye kushinda, watokao kwa yule mnyama, na sanamu yake, na kwa hesabu ya jina lake." walikuwa wanauimba wimbo ule wa Musa na wimbo wa Mwana-Kondoo, yaani, wimbo ule wa ushindi wa milele.

Katika nyakati zile za Kristo dini ile ya Kiyahudi ilichanganya mafundisho potofu pamoja na ile kweli. Wayahudi kwa sehemu fulani waliweka maagizo [amri] ya wanadamu mahali pa amri [kumi] za Mungu, yaani, mfumo ule potofu wa haki kwa njia ya matendo. Yesu akawaambia: "Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu" Mathayo 15:9.

Sabato ya Uongo [Jumapili] na Haki kwa Matendo

Kule kuweka maagizo ya wanadamu mahali pa mambo yale yaliyowekwa na Mungu huunda sehemu ya kanuni ile potofu ya wokovu kwa njia ya matendo. Sabato hiyo ya Jumapili iliyofanywa na mwanadamu na kuwekwa mahali pa Sabato ya siku ya saba iliyowekwa na Kristo ni mfano mmoja wa [kanuni] hiyo. Badiliko hilo huyaweka mamlaka ya mwanadamu juu ya mamlaka ya Kristo. Wengi hawatambui kwamba utunzaji huo wa sabato hiyo ya uongo ya siku ya kwanza ya juma badala ya Sabato ile ya kweli ya Kristo ya siku ya saba ni sehemu ya kanuni hiyo potofu ya haki kwa matendo!

Ujumbe wa Mungu wa aina tatu wa Ufunuo 14:6-12 umekusudiwa kuisahihisha kanuni hiyo potofu. Ujumbe huo unawaongoza watu katika ile haki kwa njia ya imani ambayo inaonekana katika utii kwa amri zote [kumi] za Mungu. Inairejesha mahali pake Sabato ya kweli ya Kristo kama ishara ya haki kwa njia ya imani. Hoja ya kumwabudu Kristo kama Muumbaji (Ufunuo 14:7) kinyume cha kumwabudu yule mnyama na sanamu yake (Ufunuo 14:9) kimsingi ndiyo hoja ya haki kwa njia ya imani na kiini [kitovu] cha ujumbe wa malaika yule wa tatu.

Siku moja kazi ya ujumbe huo wa aina tatu itafikia katika hatua zake za mwisho. Nchi itaangazwa kwa utukufu wa haki yake Kristo. (Linganisha Ufunuo 18:1-4 na Warumi 9:28.) Sabato itahubiriwa na kueleweka kwa maana yake ile ya kiroho yenye kina.

Idadi kubwa wataiheshimu Sabato kama ndiyo muhuri wa haki kwa njia ya imani. Wengi ambao hivi sasa wanasimama imara katika imani yao wakisadiki ya kwamba dunia hii iliumbwa kwa siku sita na ya kwamba Kristo ni Mungu kweli kweli wataipokea Sabato hiyo ya kweli ya Kristo kama ishara ya kwamba yeye ni Bwana [Yehova], Muumbaji-Mungu yule wa Mwanzo Sura ya Kwanza, na Mwokozi peke yake.

Bwana anakutaka wewe kushiriki katika ujumbe huo wa aina tatu wa siku hizi za mwisho. Nawe uwe mmoja wa hao wazishikao amri [kumi] za Mungu na imani ya Yesu. Huo ndio uamuzi wa

busara kabisa, bora na wenye heri mno ambao utapata kuufanya.

SURA YA 11

Jaribio la Mwisho: Alama ya Mnyama

=====
===

Pambano la vizazi vyote limempambanisha Kristo mwenye mfumo wake sahihi wa ibada na Shetani mwenye mfumo wake potofu wa ibada. Tangu wakati ule Lusifa (Shetani) alipofanya maasi dhidi ya Mungu, hoja ya kuwapima watu [kuwajaribu] ni ile ya kuukubali utawala halali wa Mwana wa Mungu kinyume cha ukuu wa [mamlaka kuu ya] Shetani anaodai kuwa anao.

Watu wawili wale kwa kwanza katika dunia hii, Adamu na Hawa, walikabiliwa na jaribio lilo hilo katika amri ile ya Kristo ya kuwakataza wasiukaribie mti ule wa kujulia mema na mabaya. Katika suala hilo, utii uliashiria kuitambua mamlaka kamili ya Kristo kama Muumbaji wao. Uasi ulimaanisha kuyakubali mamlaka ya Shetani aliyojinyakulia kwa kiburi chake na kujigamba, na kuyaweka mamlaka yake hayo juu ya yale ya Kristo.

Walipofukuzwa kutoka Paradiso, mti ule haukuweza kufaa tena kuwa kipimo cha kuwajaribu. Lakini njia nyingine za jaribio lilo hilo ziliendelea kwa kila mtu. Hoja ya msingi sikuzote imekuwa na itaendelea kuwa ile ile: utii kwake Kristo na Sheria yake [Amri Kumi] dhidi ya uasi [uvunjaji wa Sheria hiyo].

Kupitia katika nyakati zote za Agano la Kale mkabala unaoendelea ulikuwapo kati ya ibada ya Mungu pekee wa kweli na ibada potofu ya miungu mingi sana ya uongo. Katika nyakati za Agano Jipya Dini ile ya Kiyahudi pamoja na upagani viliupiga vita Ukristo. Baadaye, imani ile ya kwanza katika Kristo

ikapambana na mfumo ule wa upapa ambao uliweka mfumo wa matendo ili kujipatia kibali mbele za Mungu. Lakini hoja ya msingi sikuzote ilikuwa ni ile ile moja ----- ukuu halisi wa Kristo dhidi ya ukuu bandia wa Shetani.

Katika mkabala [pambano] ule wa mwisho wale Wamasalio wa Kristo [Ufu. 12:17] watapambana na mfumo potofu wa ulimwengu mzima unaowakilishwa na Babeli, yaani, ibada ya Muumbaji itapambanishwa na ibada ya Mnyama na Sanamu yake. Mwishoni hapatakuwa na kusimama katikati. Kila mmoja ataijua hoja hiyo. Je! ataukubali ukuu wa Bwana? Ama, ataukubali ukuu wa mwanadamu? Jaribio hilo linaihusisha Sabato ya kweli ya siku ya saba na kuipambanisha na sabato ya uongo ya siku ya kwanza iliyowekwa na mwanadamu.

"Na katika hili twajua ya kuwa tumemjua yeye, ikiwa tunashika amri zake [kumi]. Yeye asemaye, Nimemjua, wala hazishiki amri zake [kumi], ni mwongo, wala kweli haimo ndani yake" 1 Yohana 2:3,4.

Utii Wetu Unapimwaje?

Katika swali lake la kupenya mpaka moyoni, aliuliza hivi, "Na kwa nini mnaniita Bwana, Bwana, walakini hamyatendi nisemayo?" (Luka 6:46), Yesu aliifunua kweli hiyo. Uasi wa kudumu, unaojulikana, dhidi ya amri yo yote ya Kristo [katika zile kumi] huonyesha kukataa kwetu kumheshimu Mungu kuwa ndiye Mkuu. Hiyo ndiyo sababu ya ukengeufu huo wa kutisha wa kuiweka sabato ya siku ya kwanza ya mwanadamu mahali pa Sabato ya kweli ya siku ya saba ya Kristo.

Utunzaji sahihi wa Sabato ni ishara ya kuikubali mamlaka ile isiyo na kikomo ya Bwana, Muumbaji, na Mtakasaji wetu.

"Tena naliwapa Sabato zangu, ziwe ishara kati ya mimi na wao,... ya kuwa mimi, BWANA ndimi niwatakasaye" Ezekeieli 20:12. Kwa kinyume cha moja kwa moja, ibada ile ya jua katika siku ya kwanza ya juma ilisimama kama ishara ya mfumo wa ibada potofu wa Shetani. Akaidhihirisha mbinu yake ya kilele alipowaongoza Wakristo kuiweka Jumapili mahali pa Sabato ya kweli ya Kristo. Kwa njia hiyo akafanikiwa kuiweka siku ya JUA (SUN) mahali pa siku ya MWANA (SON), yaani, mahali pa Sabato ya siku ya saba ya Kristo.

Alijua kwamba kimojawapo cha vipigo vyake vyenye nguvu kabisa ambacho angeweza kumpiga nacho Mwana wa Mungu huyo kingekuwa kile cha kuwakengeusha watu [kuwapotosha] wasiitunze Sabato ya siku ya saba, kwa vile hiyo ndiyo ishara ya mamlaka [ukuu] ya Kristo. Kwa mwisho huo akatangaza wazo potofu kwamba Kristo alikuwa ameibadili Sabato toka Jumamosi kwenda Jumapili. Kwa njia hiyo aliwapotosha mamilioni kuamini kwa unyofu wa moyo kabisa kwamba utunzaji wa Jumapili ulikuwa ndiyo njia ya kuukiri ukuu [mamlaka] wa Bwana wetu. Lakini kule kuiacha Sabato ile ya

siku ya saba huifunua wazi tabia ya uongo huo.

Vita Kuu Kati ya Kristo na Shetani

Walakini kwa utimilizo wa Ufunuo 14:6-14, Mungu anatuma ujumbe wake maalum wa injili kuwaelemisha watu wote, ili wale wanaodhamiria kuwa wakweli kwake Kristo waweze kuona jinsi ya kufanya uamuzi wao sahihi. Hivyo Sabato ya amri ile ya nne itakuwa ndilo jaribio letu [jambo la kutupima] kuona kama sisi tutakuwa upande wake au kinyume chake Kristo.

Amri zile Kumi zinafafanua ukuu [mamlaka] wake Mungu Mwana pamoja na Mungu Baba. Amri ile ya pili, ya tatu, na ya tano, hutaja jina la "BWANA, Mungu wako." Lakini hazimtambulishi yeye kama ndiye Muumbaji. Amri ya nne, yaani, amri ya Sabato, ndiyo peke yake inayomtambulisha Bwana kama Muumbaji wa vitu vyote na kwa hiyo Mtawala halali wa vitu vyote. Hivyo, amri yake ya Sabato husimama kama muhuri, au, ishara ya ukuu wake kamili. Inazipa uhalali amri zile nyingine tisa kuwa ni amri za kweli za yule Muumbaji-Mungu wa pekee. Kama amri ya Sabato inawekwa kando, basi, Sheria ya Mungu [Amri Kumi] inafutwa yote, kwa sababu Sabato husimama kama ishara na nembo ya Muumbaji yule aliye na mamlaka ya kuzitoa amri zile nyingine [tisa].

Kinyume kabisa na msimamo huo, mamlaka ya papa inasonda kidole kwa sabato ile ya Jumapili iliyoianzisha na kuiweka mahali pa Sabato ya siku ya saba ya Amri Kumi za Mungu, kama ndiyo ISHARA au ALAMA ya mamlaka yake juu ya wanadamu wote.

Katika Katekisimu rasmi ijulikanayo kama The Abridgement of Christian Doctrine [Muhtasari wa Mafundisho ya Kikristo], iliyoandikwa na Mchungaji Henry Tuberville, katika ukurasa wake wa 58, tunalionna swali hili na jibu lake:

"Swali: Wewe unathibitishaje kwamba Kanisa [Katoliki] linao uwezo wa kuamuru [kutoa amri za] sikukuu na siku takatifu?"

"Jibu: Kwa tendo lile lile la kuibadili Sabato [Jumamosi] kuwa Jumapili."

Maneno hayo yanaweka mbele yetu mojawapo ya mambo ya kutisha mno katika utunzaji wa siku ya kwanza badala ya ile ya saba. Sabato ya Jumapili husimama kama ishara ya mamlaka ya utawala ule wa Kikatoliki. Uchaguzi huo ni zaidi ya kuamua tu kupumzika aidha Jumamosi au Jumapili. Uchaguzi huashiria uamuzi kati ya ishara mbili za mamlaka zinazopingana. Na katika jaribio lile la mwisho kila mtu atapaswa kuikubali moja au ile nyingine.

Tunapoiielewa hoja hiyo katika nuru hii, basi, tunaona kwamba ni jambo lenye matokeo ya kutisha sana. Je! tutakuwa radhi kuikubali mamlaka ile ya Roma [Vatikana] kuliko ile ya Yesu Kristo? Kule kuikanyaga Sabato ya kweli ya Kristo huwa

tunaikanyaga mamlaka ya Kristo [Waebrania 10:26-31].

Alama ya Mnyama ni Ya Kutisha Mno

Katika ujumbe wake wa mwisho, kwa uzito kabisa Bwana anaonya dhidi ya kuisujudu au kuitii mamlaka hiyo ya Mnyama au kuipokea alama (chapa) yake. Kwa kuwasihi sana wanadamu ili wamsujudu Kristo kama Muumbaji badala ya kumsujudu Mnyama na Sanamu yake, ujumbe huo wa aina tatu unakifikia kitovu cha hoja yenyewe. Unawaita watoke haraka wale Waliosalia [Wamasalio] wazishikao amri [kumi] za Mungu na imani ya Yesu. Jambo litakaloangaliwa sana katika kuuweka muhuri wa Mungu juu ya kipaji cha uso (Ufunuo 7:1-3), au kuweka Alama ya Mnyama katika kipaji cha uso au katika mkono (Ufunuo 14:9-11) litakuwa kama mtu huyo ameitunza Sabato ya kweli [Jumamosi] ama ile ya uongo [Jumapili].

"Sabato itakuwa ndilo jaribio kuu la utii wetu, kwa maana hiyo ndiyo hoja ya ile kweli inayobishaniwa hasa. Jaribio hilo la mwisho litakapoletwa juu ya watu na kuwaathiri, hapo ndipo mstari wa kugawa utakapowekwa kati ya wale wamtumikia Mungu na wale wasiomtukia. Wakati utunzaji wa sabato ile ya uongo [Jumapili] kwa kuitii sheria ya nchi [serikali], kinyume na amri ile ya nne, utakuwa ni kiapo cha utii kwa mamlaka ile inayopingana na Mungu [Mpinga Kristo], utunzaji wa Sabato ya kweli [Jumamosi], kwa kuitii Sheria ya Mungu [Amri Kumi], ni ushahidi wa utii kwa yule Muumbaji. Wakati kundi moja, kwa kuikubali ishara ya utii kwa mamlaka zile za dunia wanapokea Alama ya Mnyama, [kundi] lile jingine, likiichagua ishara ile ya utii kwa mamlaka ile ya mbinguni, watapokea Muhuri wa Mungu." ----- The Great Controversy, uk. 605.

"Kwake yeye ambaye mnajitoe nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii" Warumi 6:16. Mtu mmoja anapoitunza siku ya kwanza ya juma, yaani, Jumapili, hivi huwa anamtii nani katika kuitunza siku hiyo? Wengi kwa unyofu wao wa moyo wanafikiri kwamba wanamtii Yesu kwa kuitunza Jumapili kuadhimisha ufufuo wa Bwana wetu. Lakini katika Maandiko Matakatifu hakuna neno hata moja kutoka kinywani mwa Yesu linalomtaka mtu awaye yote kuitunza siku ya kwanza ya juma kwa sababu iwayo yote ile. Na sabato hiyo ya uongo [Jumapili] inapochukua mahali pa ile ya kweli [Jumamosi], hapo ndipo udanganyifu unakuwa umekamilika. Na iwapo mtu ye yote akiwa anajua ukweli huo lakini anaendelea tu kuitunza sabato hiyo ya uongo, basi, yeye atakuwa anapendelea kuwa mtumwa wa au anaisujudu mamlaka hiyo kuliko mamlaka ile ya Kristo.

Kwa kawaida Waprotestanti hawatambui kwamba utunzaji wa Jumapili ni ishara [alama] ya utii wao au kuisujudu kwao mamlaka ile ya papa. Wengi pasipo kujua wanaiweka amri iliyotolewa na papa juu ya amri ya Mungu.

Kitu chenye gharama kubwa mno katika ulimwengu huu wote ni

kutomtii [kumwasi] Bwana Yesu Kristo. "Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Mathayo 16:26. Mfalme Sauli alipokosa kutii amri ya Bwana, aliambiwa hivi, "Umelikataa neno la BWANA, BWANA naye amekukataa wewe" 1 Samweli 15:26.

Kabla ya kufikia mwisho watu wa Mungu wote, ambao kwa sasa wametawanyika, wataupokea ujumbe huo wa Mungu uliotolewa kwa siku zetu (Ufunuo 18:2-4). Watu wake watasimama wakiwa wameungana pamoja chini ya bendera ile yenye maandishi haya, Amri [Kumi] za Mungu na Imani ya Yesu, wakiwa wamejitoa kabisa kwa Kristo na kumtambua kama ndiye Bwana, Muumbaji, na Mwokozi wao. Watamfuata njia yote [watafuata mafundisho yake yote].

Mungu Alipotaka Uamuzi Ufanywe

Hapo zamani Eliya aliitisha mkutano mkubwa juu ya Mlima ule wa Karmeli. Hoja yenyewe ilihusu ibada ya Mungu pekee wa kweli dhidi ya ibada ya yule mungu-jua aliyejulikana kama Baali. Eliya alisema, "Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? BWANA [YEHOVA] akiwa ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! mfuateni yeye" 1 Wafalme 18:21.

Ikiwa wewe unaamini kwamba Kristo ndiye Mwokozi wako peke yake, basi, mfuata yeye na kuitunza siku yake ya saba [Jumamosi], ishara ya mamlaka yake. Ikiwa wewe unaamini kwamba mamlaka ya papa ilifanya jambo zuri katika kuuweka utunzaji wa Jumapili mahali pa Sabato ya kweli ya Kristo, basi, ifuate [mamlaka hiyo]. Ni hakika kwamba wewe hutaamua kuisujudia mamlaka ile ya Roma na kuiweka juu ya mamlaka ile ya Bwana wako!

Hoja hiyo ya Sabato itampima kila mmoja. Hebu upendo wako kwa Yesu uwe wa kweli, wenye nguvu, na ukubidisha kiasi kwamba wewe utasema hivi, "Mungu akinisaidia mimi, kuanzia sasa na kuendelea nitaitunza siku ya saba ambayo Yesu, Mwokozi wangu, aliitakasa kwa ajili yangu."

SURA YA 12

Sabato Inautia Muhuri Umoja Wako na Kristo

=====
===

Hebu fikiria Mungu akiwa amekuja kama mwanadamu, na sisi wanadamu tukiwa wapumbavu sana kiasi cha kujaribu kumfunga gerezani, naam, hata kutafuta kumwua! Yesu alimponya mtu aliyekuwa amepooza kwa miaka 38, akiufanya mwujiza huo siku ya Sabato ----- jambo halali kabisa kufanya. Lakini jambo hilo likawakasirisha mno Wayahudi hata wakamkokota na kumpeleka mahakamani "wakamwudhi [wakataka kumwua] Yesu, kwa kuwa alitenda hayo siku ya Sabato" Yohana 5:16, KJV.

Yesu hakuwa na mwanasheria wala wakili wa kumtetea mahakamani, kwa hiyo alijitetea mwenyewe. "Baba yangu anatenda kazi hata sasa, nami ninatenda kazi," akawaambia. "Basi kwa

sababu hiyo Wayahudi walizidi kutaka kumwua, kwa kuwa hakuivunja Sabato tu, bali pamoja na hayo alimwita Mungu Baba yake, akijifanya sawa na Mungu" fungu la 17 na 18.

Yeye aliendelea kujitetea mwenyewe akiwaambia kwamba kwa sababu yeye na Baba ni umoja, yeye "anatenda yale tu anayomwona Baba yake akitenda," hata kwa upeo ule wa kuweza kuwafufua wafu. "Siyatafuti mapenzi yangu mimi, bali mapenzi yake aliyenipeleka." Fungu la 30. Kwa maneno mengine, Yesu mwenyewe alikuwa mikononi mwa mapenzi ya Baba yake. Sabato ni siku inayotufundisha kuhusu uweza wa Baba yetu, kwa kuwa "amefanya ukumbusho wa matendo yake ya ajabu; BWANA ni mwenye fadhili na rehema" Zaburi 111:3,4. Yesu alipokuwa mikononi mwa mapenzi ya Baba yake, alitenda "kazi" zile zile alizotenda Baba yake. Kwa nini basi, asiweze kumponya mtu yule aliyepooza siku ile ya Sabato? Tendo lile lilikuwa lenye "fadhili na rehema," au sivyo?

Kuna mbaraka wa pekee ulioambatanishwa na Sabato, kwa sababu "Mungu akaibarikia siku ya saba" Mwanzo 2:2,3. Wanadamu wanaweza kubarikiwa na Bwana katika siku yo yote ya juma. Naam, "yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki" kila siku katika juma (Mathayo 5:45). Bwana yu karibu sikuzote kutubariki. Lakini kuna mbaraka wa pekee wa Sabato kulingana na Neno la Mungu. Mbaraka huo huambatana tu na Sabato. Haujawekwa juu ya siku nyingine yo yote, kwa hiyo, hauwezi kupatikana mahali pengine po pote. Watu wengi hukana kuwako kwa mbaraka huo wa pekee kwa sababu tu hawaujui. Lakini ni upumbavu kukana kile ambacho mtu hakijui!

Faida Isiyopimika ya Kuwekwa Huru Mbali na Maovu

Mbaraka huo wa pekee ni kwa ajili ya nani? "Mungu, akiisha kumfufua mtumishi wake Yesu, alimtuma kwenu ninyi kwanza, ili kuwabarikia kwa kumwepusha kila mmoja wenu na maovu yake" Matendo 3:26. Mungu huwabariki watu si kwa sababu wao ni wema, bali ili wapate kuwa hivyo. Kuwa mtumwa wa maovu [dhambi] ni kuwa chini ya laana ya utumwa huo. "Maovu yangu yamenipata, wala siwezi kuona" Zaburi 40:12. Maovu ni chimbuko la huzuni yote na hatia ambazo ulimwengu huu unajua. Roho Mtakatifu, kupitia kwa Sabato hiyo, anatuokoa sisi kutokana na laana ya utumwa ule, kwa kutukumbusha kila juma ya kuwa "Bwana ni mwenye fadhili na rehema." Sabato inatangaza habari ya uweza wa Mungu, uweza ule unaotufanya sisi kuwa watu wapya kabisa ndani yake Kristo.

Watu huzungumza juu ya "Sabato ya Wayahudi," "Sabato ya Waislamu," "Sabato ya Wapuyuritani (Puritan)," na kadhalika. Lakini Sabato pekee ambayo Biblia inaongea habari zake ni "Sabato ya Bwana," "Sabato zangu," "Siku ya utakatifu wangu." Sisi inatupasa kuitunza raha yake hiyo.

Sabato ni Ishara Halisi ya Msalaba

Mamilioni ya watu hupenda kufanya ile iitwayo 'alama ya msalaba." Wanasimika misalaba juu ya mapaa ya makanisa yao, wanaitundika kwenye kuta, hata kuivaa shingoni mwao. "Ishara ya msalaba" ndiyo nembo yao, wakati mwezi ndiyo "ishara" au nembo ya Uislamu.

Jambo hilo linaweza kugeuka kwa urahisi na kuwa aina fulani ya ibada ya sanamu, ambayo Agano Jipya inaipinga. Vitu, picha, mahali, si vitakatifu; Mungu peke yake ndiye mtakatifu, walakini yeye ameibariki na kuitakasa sehemu fulani ya wakati wetu inayojulikana kama Sabato. "Mungu ni upendo," na yeye ndiye Muumbaji na Mkombozi wetu pia. Upendo wake unadhihirishwa pale msalabani ambapo Mwana wa Mungu alijitoa nafsi yake kwa ajili ya dhambi zetu ili kutukomboza sisi, na "neni la [kuhubiri habari za] msalaba... ni nguvu ya Mungu" 1 Wakorintho 1:18.

Kwa kuwa Sabato ni ishara ya uweza wake wa uumbaji, na kwa kuwa uweza ule ule unafanya kazi kuu kwa wokovu wetu, tunaona kwamba Sabato ni ishara ya kweli ya msalaba. Uweza uliodhihirishwa pale msalabani ni uweza ule unaovishikilia vitu vyote ulimwenguni. Ndani yake Kristo, tunakuwa "kiumbe kipya, "Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeneza" Waefeso 2:10. Kusulibiwa pamoja na Kristo maana yake kujitoa nafsi kabisa, tukikiri kwamba sisi wenyewe hatufai kitu, na kuweka imani yetu kamili ndani ya Kristo. Ndani yake tunapumzika; ndani yake tunaipata Sabato. Kuitunza Sabato ni ishara ya kuwa sisi tumepatanishwa na Mungu, ya kuwa sisi tunapumzika mbali na dhambi katika kazi yake ile kamilifu ya ukombozi.

Kuna uponyaji kwa ajili yetu katika majeraha yake Kristo. Kuna mbaraka kwa ajili yetu katika laana ile aliyoichukua badala yetu. Twawezaje kwa uchoyo wetu kuzuia kitu cho chote kwake wakati yeye alitoa vyote kwa ajili yetu? Mtunzaji wa Sabato wa kweli haoni fahari katika kitu kingine cho chote "ila msalaba wa Bwana wetu Yesu Kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibiwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu" Wagalatia 6:14. Paulo aliposema maneno haya katika fungu lile la 17 kuwa alichukua katika mwili wake "chapa [alama] zake Bwana Yesu," hakuwa na maana ya kwamba alikuwa amejichanja chale mwilini mwake, wala kwamba alikuwa anavaa msalaba wa dhahabu shingoni mwake. Alimaanisha kwamba maisha yake yote, roho, nafsi, na mwili, vilikuwa vimetolewa kabisa kumtumikia Kristo.

Sabato na Evalusheni

Wanaevalusheni wanatuambia kwamba sisi ni wanyama waliokua kwa hali ya juu. Lakini basi, wanyama si viumbe vya kiroho.

Kristo anatuambia kwamba "Mungu ni Roho" Yohana 4:24. Je, hiyo ina maana kwamba yeye ni kivuli tu au wingu, kwamba yeye si nafsi halisi? Hasha! Vitu vile tu vilivyo halisi ni vile vilivyo vya kiroho ----- vitu vyote vyenye mwili vinaweza kufutiliwa mbali kwa dakika moja kwa moto, mafuriko, au mabomu ya nyuklia. "Ikiwa uko mwili wa asili, na wa roho pia uko" 1 Wakorintho 15:44. Ni vitu vya kiroho tu vitakavyodumu milele zote.

Kwa vile Mungu ni Roho, basi, pumziko alilochukua baada ya kuumba mbingu na nchi lilikuwa ni pumziko la kiroho. Haikuwa kwamba alikuwa amechoka kimwili, kwa maana "Mungu wa milele, BWANA, Muumba miisho ya dunia, hazimii, wala hachoki" Isaya 40:28. Uumbaji haukuwa kazi ya kutumia mwili; ilikuwa kazi ya kiroho. Mungu alisema, na ikawa [Zaburi 33:6,9].

Kwa hiyo, kuitunza Sabato ya Mungu, au raha yake, ni kuifurahia raha yake ya kiroho. Wakati ni kweli kwamba hatutakiwi kuendelea kufanya kazi zetu za kimwili za kila siku katika siku ile takatifu, pia ni kweli kwamba pasipo kuwa na pumziko la kiroho hakuna utunzaji wa Sabato.

Kabla dhambi haijaiingia katika dunia hii, Adamu alikuwa na kazi ya kufanya, lakini haikuwa kazi ya kuchosha sana. Kazi yenyewe si sehemu ya laana ambayo ililetwa na dhambi, bali uchovu mwingi kutokana na kazi hiyo huo ndio [laana]. Ni baada tu ya dhambi kuja ndipo Bwana aliposema, "Kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi" Mwanzo 3:19. Kama mwanadamu angekuwa hajatenda dhambi, Sabato ingekuwa imetunzwa, si kama pumziko kwa miili iliyochoka, bali kama wakati wa pekee wa kuwasiliana na Mungu. Kwa hiyo, Sabato ni kiungo kinachotuunganisha sisi na Paradiso ile iliyopotea na Paradiso ile itakayorejeshwa; ni ushahidi wa kila juma unaoshuhudia kwamba mwanadamu ni zaidi ya mnyama. Yeye ni mtoto wa familia ile ya Mungu.

Je! Serikali Iwalazimishe Watu Kuitunza Sabato?

Endapo Sabato ingekuwa imekusudiwa tu kuleta pumziko la kimwili, hapo ingekuwa ni busara kwa serikali za kidunia kutunga sheria zinazowataka watu kuitunza. (Wengine wanataka serikali itunge sheria kama hizo ili kuwalazimisha watu kuitunza Jumapili, Jumamosi, au Ijumaa.) Lakini kwa vile Sabato ni pumziko la kiroho, hakuna hata mmoja anayeweza kulazimishwa kuitunza. "Mambo ya kiroho hufungamana na Mungu peke yake, ambaye [yeye mwenyewe] ni Roho. Ni Roho wa Mungu tu awezaye kutoa pumziko kama hilo. Wala yeye hatawaliwi na mahakama zo zote wala mabunge. Mungu hatumii ulazimishaji, wala hajatoa madaraka hayo kwa mtu ye yote yule, kanisa lo lote lile, wala kwa serikali yo yote kuutumia [ulazimishaji huo] kwa niaba yake.

Ulazimishaji wo wote au utumiaji nguvu katika mambo ya kidini ni ushahidi wa hakika kwamba dini hiyo inayolazimishwa ni ya

uongo. Ni kukiri waziwazi kwamba [dini] hiyo haina uwezo wote wa kuushawishi moyo wa mwanadamu. Kristo anasema kwamba yeye "[a]tawavuta wote" kwake; lakini yeye hajaribu kamwe kuwalazimisha. Yeye ndiye Mchungaji mwema; mchungaji hawaswagi kamwe kondoo wake!

Kama ishara ya pumziko lile la kiroho, Bwana anatuamuru sisi ya kuwa katika siku hiyo ya Sabato "usifanye kazi yo yote, wewe." Kwa nini? Sababu mojawapo ni kukupa nafasi ya kujifunza habari zake bila kuingiliwa kila wakati na masumbufu ya ulimwengu huu wala wasiwasi. Jambo hilo ni la maana; na hiyo ndiyo mojawapo ya sababu kwa nini Sabato ni mbaraka hivyo "kwa mwanadamu," ni zawadi hasa. Endapo Mungu kwa busara yake na upendo wake asingekuwa ametuamuru sisi kupumzika kwa kuacha kuzifanya kazi zetu siku ya Sabato, huenda asingekuwako mtu hata mmoja ambaye angepumzika siku hiyo ya Sabato. Uchu wa asili ulio ndani ya mwanadamu wa kuchuma mali na hofu yake ya kuogopa njaa vingemfanya aweze kubanwa sana kiasi cha kuendelea kufanya kazi siku saba kwa juma, na aidha uchoyo wake huo au hofu yake hiyo ingemfanya awe chini ya mahangaiko hayo.

Lakini sababu ya maana zaidi inayoonyesha kwa nini Bwana ametuamuru sisi kutofanya kazi yo yote siku hiyo ya Sabato ni kwamba sisi tunakumbushwa kwamba Mungu ndiye anayetupatia mahitaji yetu yote ya kimwili na ya kiroho. Kufungamanishwa kwa karibu sana na "kuikumbuka" hiyo Sabato ni maneno yafuatayo yanayotukumbusha: "Bali utamkumbuka BWANA, Mungu wako, maana ndiye akupaye nguvu za kupata utajiri" Kumbukumbu la Torati 8:18. Huenda sisi tusitambue hilo, au huenda tukaweza kulisahau kwa urahisi (kama hatuna Sabato), lakini ni jambo la kweli kwamba hakuna hata mmoja wetu ambaye angeweza kula kipande cha mkate [chakula] kama kisingekuwa zawadi ya neema ya Mungu kwetu. "Ndani yake tunaishi, tunakwenda, na kuwa na uhai wetu" Matendo 17:28. Kila boflo ya mkate imepigwa chapa ya msalaba wake Kristo. Kila mtu, awe mtakatifu au mwenye dhambi, anapokula mkate [chakula] wake wa kila siku anapata lishe yake kutokana na mwili na damu ya Mwana wa Mungu. Sisi tunamtegemea kabisa Bwana kwa mahitaji yetu ya kila siku, ingawa tunafanya kazi ya sulubu au kulima mashamba yetu ili kujipatia mahitaji hayo. "Nguvu ya kupata mali" inatoka kwake peke yake.

Hoja za Shetani Tayari Zimeshindwa

Ukweli huu wa maana huyaondolea mbali milele mashaka yote ambayo Shetani anatushawishi kuwa nayo kama sisi tunaweza "kumudu" kuitunza Sabato hiyo. Shetani anayo hoja tayari kwa ajili yetu mara tu tunapojifunza ukweli huo, anasema: "Unawezaje kuitunza Sabato hiyo? Achana na wazo hilo la kipumbavu! Unawezaje kuwa na maisha mazuri usipofanya kazi siku ya Jumamosi? Hiyo ndiyo siku ya ulimwengu yenye shughuli [biashara] nyingi mno! Unaweza kupoteza kazi yako." Sabato yenyewe inatoa jibu lililo wazi: Inafundisha kumtegemea Mungu kabisa, ambaye uweza wake uliitoa dunia hii kutoka pasipo kitu,

tena ni [uweza] huo ambao mpaka leo unaishikilia [angani]. Upendo wake kwa watoto wake unalingana kabisa na uweza wake wa kuwatunza.

Kwa vile sisi tunamtegemea Bwana kabisa kwa kila kipande cha chakula tunachokula, Sabato ni ungamo [kukiri] letu kwake kwamba sisi tunamwamini na kusema "Asante." Hakuna mtu hata mmoja aliyekufa kwa njaa kwa sababu alimtii Bwana kwa kuitunza Sabato yake; na kama ukweli ungejulikana, Bwana hajamwacha kamwe mtu hata mmoja aliyetumia imani yake kwake kwa kuchagua kuitunza [Sabato hiyo].

Ukweli huo pia unatatua tatizo la "kazi ya dharura" siku ile ya Sabato wakati ule wa mavuno au shinikizo la kibiashara. Iwapo mkulima anajaribiwa kuvuna mazao yake siku ya Sabato, atakumbuka kwamba Mungu yule yule aliyeyawezesha mavuno hayo kukua na kukomaa anaweza kabisa kuyatunza [yasiharibike] kama jibu kwa sala ya mtoto wake. Imani kwa Mungu haimpi mtu ruhusa [leseni] ya kuzivunja amri zake [kumi] kutokana na hofu zake za kibinadamu. (Naam, kazi zile za rehema na huruma kwa wagonjwa na wale wanaoteseka sikuzote zinaafikiana kabisa na utunzaji wa Sabato.)

Ni mpango wa ajabu jinsi gani alio nao Mungu kwa ajili ya kuwafundisha watu wake kumwamini yeye! "Maana sisi tulioamini tunaingia katika raha ile [ya Sabato]" Waebrania 4:3. Hali yetu ya asili, yenye dhambi tunapokuwa "wafu kwa sababu ya makosa yetu" ni ile iliyo na hisia ya kufanya-sisi-wenyewe ambayo ni [hisia] ya yatima. "Mimi najiongoza mwenyewe!" au "Mimi naweza kujitunza mwenyewe!" ni lugha ya moyo uliojaa kiburi. Ni lugha ya Farao aliyejigamba, akisema, "BWANA ni nani, hata niisikilize sauti yake?" Kutoka 5:2. Lakini Farao alishushwa chini kabisa, kwa maana "njia ya mwanadamu haimo katika nafsi yake; kuelekeza hatua zake si katika uwezo wa mwanadamu" Yeremia 10:23. Sisi ni lazima tupangwe [tufanywe] kuwa watoto" wa familia yake Mungu.

Farao alijifunza fundisho lake kwa njia ngumu ----- kuzama chini ya Bahari ile ya Shamu. Wewe na mimi twaweza kujifunza kwa njia rahisi ----- kwa kuitunza Sabato ya Bwana. Kabla hatujajifunza fundisho hilo la imani, mambo yote tufanyayo hutokana na nafsi zetu. "Matendo ya mwili" ni dhambi tupu, kwa maana "matendo yetu yote ya haki yamekuwa kama nguo iliyotiwa unajisi" Isaya 64:6.

Lakini tunapoitumia imani yetu, hapo ndipo tunakoma "na kuacha [kutegemea kazi] matendo yetu kwa sababu tunaingia "katika raha yake" Waebrania 4:10. Ndipo Bwana anapofanya kazi ndani yetu kutaka kwetu na kutenda kwetu, kwa kulitimiza kusudi lake jema [Wafilipi 2:13]." Kazi [matendo] zetu zote zinapofanyika ndani yake, ni njema. Hiyo ndiyo raha kweli. Inakuja sisi tunapotambua kwamba yule Neno aliyefanya mbingu na nchi, tena, yule anayezishikilia mahali pake ndiye pia aliyetukomboza sisi kila mmoja peke yake. Raha hiyo huja kwa njia ya Sabato. Uweza ule ule ulioitakasa Sabato hiyo ndio unaomtakasa yule anayemwamini Kristo.

Hitimisho

Hii ndiyo maana tulisema mwanzoni mwa kitabu hiki kwamba iwapo ungekuwa umepewa zawadi ya lori lililojazwa dhahabu, kwako isingekuwa baraka sana kama ilivyo ile ya Sabato. Hiyo inakuletea kile ambacho dhahabu haiwezi kamwe kukuletea ----- yaani, furaha. Kichwa cha Zaburi 92 kwa lugha ya Kiebrania ni "Wimbo kwa ajili ya Sabato."

Ni neno jema kumshukuru BWANA,
Na kuliambia jina lako, Ee Uliye juu.
Kuzitangaza rehema zako asubuhi,
Na uaminifu wako wakati wa usiku.
Kwa chombo chenye nyuzi kumi,
Na kwa kinanda, Na kwa mlio wa kinubi.
Kwa kuwa umenifurahisha, BWANA,
Kwa kazi yako; nitashangilia
Kwa ajili ya matendo ya mikono yako.

Tunapolemewa na majaribu pamoja na maonjo, yatupasa kutakafari juu ya "kazi [matendo] yake," na ndipo tutakuwa na furaha tena. Uweza ule mkuu unatumika kutuokoa sisi. Hakuna neno gumu kwa Bwana, wala hakuna mamlaka yo yote inayoweza kumpinga yeye. Kristo ame"zivua [ameziharibu] enzi (na mamlaka)" Wakolosai 2:15, KJV. Tunapokaa katika mamlaka yake hayo, basi, ushindi wetu unakuwa umekwisha patikana tayari.

Kwa sababu hiyo, Sabato ni muhuri wa kiumbe kipya ndani ya Kristo, yaani, yule aliyekwisha kuunganishwa naye kwa imani. Akiwa amezaliwa kama kiumbe kinachotokana na mavumbi, sasa anakuwa mshirika aliyezaliwa mara ya pili wa familia ile ya mbinguni. Kwa hiyo Sabato ndiyo "Muhuri wa Mungu" ambao unawekwa juu ya "vipaji vya nyuso" za watumishi wa Mungu katika siku hizi za mwisho (Ufunuo 7:1-4). Ilitoka Paradiso na inawatia alama wale ambao wamekusudiwa kuishi milele katika Paradiso [mpya]. Wataendelea kukusanyika pamoja Sabato hata Sabato milele hata milele, hapo ndipo watakapo"imba kwa furaha" kwa sababu ya kile alichowatendea Mwokozi wao, wakisema:

Astahili Mwana-Kondoo aliyechinjwa kuupokea uweza, na utajiri,
na hekima, na nguvu, na heshima, na utukufu, na baraka.

NYONGEZA

BIBLIA ISEMAVYO JUU YA KUITUNZA SABATO

Tunapaswa kutumika na kufanya kazi yetu yote kwa siku zile sita za juma. Kutoka 20:9.

Hatupaswi kufanya kazi yo yote siku ya Sabato. Kutoka 20:10.

Hata wafanya kazi wetu [watumishi] wanapaswa kuruhusiwa kupumzika siku ya Sabato. Kutoka 20:10.

Utunzaji wetu wa Sabato unatakiwa kuwa ushuhuda kwa wageni wetu wanaotutembelea na wale tusiowajua. Kutoka 20:10.

Yatupasa kuwafundisha watoto wetu juu ya utunzaji wa Sabato kwa uaminifu. Kutoka 20:10; Kum. 6:6,7.

Hata katika nyakati tunaposongwa sana, tunapaswa kuitunza Sabato. Kutoka 34:21.

Siku ya Ijumaa ndiyo siku ya maandalio ambayo tunapaswa kufanya ili kuiweka nyumba yetu katika hali ya usafi na kufanya mapishi yetu kama maandalizi kwa kupumzika siku ya Sabato.

Kutoka 16:22,23.

Wafuasi wa Kristo baada ya kifo chake walifanya maandalizi yote siku ile ya Ijumaa.

Luka 23:50-56.

Sabato huanza jua linapokuchwa [linapozama] siku ya Ijumaa jioni. Mwanzo 1:5; Lawi 23:32.

Angalia jinsi Yesu na wanafunzi wake walivyotambua kuwa Sabato ilikwisha jua lilipokuchwa [lilipozama] siku ile ya Jumamosi jioni. Marko 1:23, 32-34.

Hatutakiwi kununua wala kuuza siku ya Sabato. Nehemia 10:31.

Utunzaji wa Sabato ni pamoja na kukusanyika pamoja kwa ibada na ushirikiano wa kiroho. Lawi 23:3 ("kusanyiko takatifu" ni kuwaita watu mahali pamoja, au ni mkutano). Angalia pia Waebrania 10:23-25.

Zaburi 92 isomwe kwa makini, kwa maana inaorodhesha kinagaubaga mibaraka ile inayoweza kupatikana kwa kuitunza Sabato hiyo.

Sehemu ya Sabato iliyo ya maana kuliko zote ni ile furaha inayoletwa nayo moyoni kwa njia ya kuzungumza na Mungu pamoja na wale wanaompenda. Zaburi 111:2-4. Furaha ya kuangalia uzuri wa kazi zake katika maumbile ni jambo halali siku ya Sabato.

Utunzaji wa Sabato uletao furaha ni pamoja na huduma yetu kwa maskini, wapweke, wazee vikongwe, wagonjwa, na wale wanaoteseka. Isaya 58:6-14. Kama watu wote wa Mungu wangeitunza Sabato kweli kweli, basi, ingesaidia sana kupunguza mateso wanayopata watu ulimwenguni humu. Mathayo 12:12.

Yule anayemwamini Kristo anatambua kwamba saa za Sabato ni tofauti na saa nyingine zo zote za juma ----- saa hizo ni "takatifu." Kutoka 20:8; Ezekieli 44:24; Kum.5:12.

Magazeti makubwa yanayotolewa mara kwa mara yaliyojaa mambo ya kidunia, magazeti ya kawaida ya kila siku, habari za kidunia zinazotangazwa na TV, Video na Redio, mambo hayo yote yanapaswa kuwekwa kando siku ya Sabato.

Hata mazungumzo tu ya biashara yaepukwe. Sabato ni siku ya mbingu kuwa hapa duniani. Isaya 58:13.

Mbali na kuwa hali ya kuleta maudhi sana, utunzaji wa Sabato huleta furaha, kwa kuwa ni kuishi katika hali ya umoja na mbingu. Isaya 58:14.

NOTES TO THE PUBLISHER

THE LORD'S DAY - PICTURES FOR INCLUSION

(SCRIPT ON THE REVERSE SIDE OF THE PICTURE)

PICTURE AND SCRIPT ON PAGES 16-17. SWAHILI SURA YA 2.

Siku ya Sabato ni siku ya mapumziko ambayo sisi tunaweza kuitumia

kwa kutafakari uzuri wa uumbaji wake Mungu.

PICTURE AND SCRIPT ON PAGES 28-29. SWAHILI SURA YA 4.

Sabato, pamoja na amri zile nyingine tisa, alipewa Musa Mlimani Sinai.

Walakini, amri hizo [kumi] zilitolewa kwa Musa mbali na Sheria

ya Musa,

nazo zilikuwa ndiyo sehemu peke yake ya Maandiko iliyoandikwa kwa kidole

cha Mungu (Kutoka 31:18).

PICTURE AND SCRIPT ON PAGES 30-31. SWAHILI SURA YA 4.

Yesu Kristo, Muasisi wa dini ya Kikristo, ndiye pia Muasisi wa Sabato.

Aliifanya iweko wakati ule alipoiumba Dunia hii kwa siku sita na

kupumzika ile ya saba.

PICTURE AND SCRIPT ON PAGES 46-47. SWAHILI SURA YA 6.

Utunzaji sahihi wa Sabato ya siku ya saba (Jumamosi), yaani, siku ya

mapumziko iliyotengwa na Kristo katika Maandiko, utaleta amani na furaha kwa wote

katika familia yao.

PICTURE AND SCRIPT ON PAGES 56-57. SWAHILI SURA YA 8.

Sheria ya kwanza kabisa katika historia iliyowataka watu kuabudu katika

siku ya kwanza ya juma ni ile iliyotangazwa na Mfalme wa Kirumi

Konstantino mwaka 321 B.K.

PICTURE AND SCRIPT ON PAGES 60-61. SWAHILI SURA YA 9.

Malaika watatu wanaoruka katikati ya mbingu huwakilisha kazi ya ulimwengu

mzima ya wajumbe wa Kristo wanaoipeleka "habari njema" kwa kila taifa na

kila jamaa ulimwenguni muda mfupi tu kabla ya marejeo yake Kristo. Ni

mpango wa Mungu kwamba kila mmoja apate kuusikia ujumbe huo wa neema

yake. Kazi hiyo kubwa itakapokwisha, Kristo atakuja.

CHART ON PAGES 70-71.

SWAHILI SURYA YA 10.

| | | | |
|---|-----------|----------|----------------------|
| 1 | 2 | 3 | 4 |
| 5 | | | |
| 6 | 7 | Majuma 7 | Majuma 62, au Juma 1 |
| Miaka 49 | Miaka 434 | Miaka 7 | |
| Muda wa Majuma 70 umeamriwa juu ya watu wako - Miaka 490. | | | Miaka 1,810 |

SIKU 2,300

Miaka hiyo mingi sana, yaani, kipindi cha unabii kirefu kupita vyote katika Biblia, kwa mujibu wa unabii wa Danieli kilikusudiwa kuanza "tangu kuwekwa amri ya kutengeneza na kuujenga upya Yerusalemu," mpaka wakati wa kutakaswa Patakatifu. Amri ya kuujenga upya Yerusalemu ilitolewa mwaka ule wa 457 K.K. Majuma yale sabini (miaka 490) yaliamriwa kwa ajili ya Wayahudi, na ilikuwa mwisho wa kipindi kile katika mwaka ule wa 34 B.K. injili ilipoanza kuhubiriwa kwa Mataifa. Tangu mwanzo wa kipindi kile mpaka kufikia kwa Masihi Mkuu yalitakiwa kupita majuma sitini na tisa (miaka 483). Wakati ule ule hasa uliotabiriwa, katika majira ya kuchipua ya mwaka wa 27 B.K., Yesu alibatizwa na Yohana Mbatizaji katika Mto ule wa Yordani; naye akiwa ametiwa mafuta na Roho Mtakatifu [Matendo 10:38], alianza kazi yake miongoni mwa watu. "Na kwa nusu ya juma hilo" (miaka mitatu na nusu baadaye) Masihi akakatiliwa mbali [akauawa kikatili]. Kipindi chote cha miaka 2,300 kilianza mwaka 457 K.K. na kumalizika mwaka 1844 B.K., wakati Hukumu ya Upelelezi ilipoanza mbinguni.

PICTURE AND SCRIPT ON PAGES 80-81.

SWAHILI SURA YA 11.

Yatupasa kujifunza Maandiko ili kuyajua na kuyafuata mapenzi ya Mungu.

PICTURE NA SCRIPT ON PAGES 84-85.

SWAHILI SURA YA 12.

"Pendo ndilo utimilifu wa Sheria [Amri Kumi]". Tunapotafakari juu ya kafara

ya Kristo iliyotolewa kwa ajili yetu, mioyo yetu inajazwa na upendo kwa Mungu

na Sheria yake [Amri Kumi]. Tunatamani kuzishika amri zake [kumi], na,

kwa njia ya imani, uweza wake unatolewa kwetu.

